

**TAFSIRI KATIKA USHAIRI: ULINGANISHO NA
ULINGANUZI WA TAFSIRI MBILI ZA *UTENZI WA*
*OMAR KHAYYAM***

MWELELE MAGEMBE

SHAHADA YA UMAHIRI KATIKA FASIHI YA

KISWAHILI

CHUO KIKUU CHA DODOMA

OKTOBA, 2018

TAFSIRI KATIKA USHAIRI: ULINGANISHO NA ULINGANUZI

WA TAFSIRI MBILI ZA *UTENZI WA OMAR KHAYYAM*

NA

MWELELE MAGEMBE

**TASNIFU IMETOLEWA KWA AJILI YA KUKAMILISHA
MAHITAJI YA SHAHADA YA UMAHIRI KATIKA FASIHI YA
KISWAHILI**

CHUO KIKUU CHA DODOMA

OKTOBA, 2018

IKIRARI

NA

HAKIMILIKI

Mimi, **Mwelele Magembe** ninathibitisha kwamba tasnifu hii ni kazi yangu asilia; na kwamba, haijawahi kuwasilishwa na wala haitawasilishwa katika Chuo Kikuu kingine ndani na nje ya nchi kwa ajili ya kutunukiwa shahada inayofanana na hii au nyingine yoyote.

Saini.....

Hairuhusiwi kuiga, kuzalisha, kunakili, kutafsiri ama kusambaza sehemu yoyote ya tasnifu hii kwa namna yoyote ile bila kibali cha maandishi kutoka kwa mwandishi wa tasnifu hii au Chuo Kikuu cha Dodoma.

ITHIBATI

Aliyesaini hapa chini anathibitisha kwamba ameisoma tasnifu hii inayoitwa *“Tafsiri katika Ushairi: Ulinganisho na Ulinganuzi wa Tafsiri Mbili za Utenzi wa Omar Khayyam”* na anapendekeza ikubaliwe na Chuo Kikuu cha Dodoma kwa minajili ya kutunukiwa Shahada ya Umahiri katika Fasihi ya Kiswahili ya Chuo Kikuu cha Dodoma.

.....
Dkt. Athumani S. Ponera

(Msimamizi)

Tarehe.....

SHUKURANI

Kwanza, ninatoa shukurani zangu za pekee kwa Mungu kwa kunijaalia afya njema na kuniwezesha kufanya utafiti huu. Pili, natoa shukurani zangu za dhati kwa msimamizi wangu, Dkt. Athumani S. Ponera, ambaye licha ya majukumu mengi aliyonayo, lakini alijitoa kuniongoza na kunishauri hatua kwa hatua hadi kukamilisha kazi hii. Asante mwalimu wangu, moyo na nia ya kusaidia wengine wafikie malengo yao udumishe. Mungu wa Mbinguni akubariki na aendelee kukulinda daima. Pia, ninawashukuru wahadhiri wangu wote, Dkt. Athumani S. Ponera, Dkt. Ester Masele, Dkt. Zuhura Badru, Dkt. Rashid Chuachua, na Bwana Aginiwe Sanga kwa mafundisho na miongozo yao kwa kipindi chote nilichokuwa darasani.

Tatu, natoa shukurani zangu kwa wazazi wangu, Mzee Masolwa Kulwa na Martha Shija, kwa kunizaa na kunilea katika maadili mema na moyo wa kujituma. Asanteni sana Mungu wangu wa Mbinguni aendelee kuwalinda na kuwatunza daima.

Nne, ninazielekeza shukurani za pekee kwa mke wangu, Maria Zacharia, pamoja na watoto wangu Joshua, Joseph, Zacharia na Zita. Asanteni kwa uvumilivu wenu mkubwa mliouonesha kwangu kwa kipindi chote cha masomo yangu

Tano, ninawashukuru wanafunzi wenzangu wa Shahada ya Umahiri 2016-2018, hasa kundi langu la majadiliano. Hawa ni Mzee Khatib Nassoro, Kaponda George, Respicius Renatus, Zahoro Selandi na Birigitha John.

TABARUKU

Naitabaruku kazi hii kwa baba yangu mdogo, marehemu Mhoja Tiluli Bundala.
Mungu aendelee kukupa amani ya milele mahali ulikolala. Kazi uliyoianzisha ndani
yangu si ndogo!

IKISIRI

Tasnifu hii inahusu tafsiri katika ushairi kwa kulinganisha na kulinganua tafsiri mbili za *Utenzi wa Omar Khayyam*. Tafsiri hizi ni ile ya Kiingereza ya Edward FitzGerald chapa ya kwanza na ile ya Kiswahili ya Shaaban Robert aliyoitafsiri kutoka tafsiri ya Edward FitzGerald. Tatizo lililomsukuma mtafiti kufanya utafiti ni kuziba pengo la kiutafiti juu ya tafsiri katika ushairi, hasa tafsiri ya tafsiri. Mtafiti alikuwa na malengo mahsusi matatu. Mosi, kufafanua mbinu zilizotumiwa na Edward FitzGerald na Shaaban Robert kutafsiri *Utenzi wa Omar Khayyam*. Pili, kulinganisha na kulinganua tafsiri mbili za *Utenzi wa Omar Khayyam* ile ya Kiingereza ya Edward FitzGerald na ile ya Kiswahili ya Shaaban Robert. Na, tatu, kutathmini kuwapo kwa mwachano kati ya tafsiri mbili za *Utenzi wa Omar Khayyam*. Data za utafiti zilikusanywa maktabani na uwandani. Utafiti uliongozwa na nadharia za ulinganisho wa kidhima na ulinganisho wa umbo la matini.

Utafiti umegundua kuwapo kwa ulinganifu na ulinganuzi katika tafsiri kama matini imetafsiriwa kwa zaidi ya lugha moja. Pia, utafiti umegundua kuwa mwachano uliopo katika tafsiri umesababishwa na ugumu wa kutafsiri utanzu husika, tofauti za kiisimu, kiutamaduni mira na desturi na tofauti za nyakati.

Mchango mpya ulioibuliwa na utafiti huu ni: kubainishwa kwa mwachano wa tafsiri katika ushairi endapo matini imetafsiriwa kwa lugha zaidi ya moja; kubainishwa kwa sababu za mwachano huo; pamoja na kuyakinisha jinsi nadharia za ulinganifu zinavyofaa katika kulinganisha na kulinganua tafsiri za fasihi andishi.

YALIYOMO

IKIRARI NA HAKIMILIKI	i
ITHIBATI	ii
SHUKURANI	iii
TABARUKU	iv
IKISIRI.....	v
YALIYOMO	vi
ORODHA YA VIFUPISHO VILIVYOTUMIKA	x
SURA YA KWANZA.....	1
UTANGULIZI	1
1.1 Ufafanuzi wa Istilahi Muhimu Zilizotumika katika Utafiti Huu	1
1.1.1 Tafsiri	1
1.1.2 Mfasiri	1
1.1.3 Ulinganisho na Ulinganuzi.....	1
1.1.4 Matini Chanzi.....	2
1.1.5 Matini Lengwa	2
1.1.6 Tafsiri Nzuri/Mbaya.....	2
1.1.7 Matini za Kishairi.....	3
1.1.8 Lugha Chanzi	3
1.1.9 Lugha Lengwa.....	3
1.1.10 Utamaduni	4
1.1.11 Itikadi	4
1.1.12 Mila na Desturi.....	4
1.1.13 Mazingira	5
1.1.14 Mtindo	5
1.1.15 Muundo	5
1.1.16 Jamii ya Watafsiriwa.....	6
1.2 Usuli wa Tatizo la Utafiti	6
1.3 Tamko la Tatizo la Utafiti	8
1.4 Malengo ya Utafiti	9
1.4.1 Lengo la Jumla	9
1.4.2 Malengo Mahsusi	9

1.5 Maswali ya Utafiti.....	10
1.6 Manufaa ya Utafiti	10
1.7 Muhtasari wa Sura ya Kwanza.....	10
SURA YA PILI.....	11
MAPITIO YA MAANDIKO NA KIUNZI CHA NADHARIA.....	11
2.1 Utangulizi.....	11
2.2 Mapitio ya Maandiko	11
2.2.1 Maandiko Kuhusu Umuhimu na Maendeleo ya Tafsiri Ulimwenguni.....	11
2.2.2 Maandiko Kuhusu Tafsiri Katika Fasihi	14
2.2.3 Maandiko Kuhusu Tafsiri Katika Ushairi na Changamoto Zake.....	16
2.2.4 Maandiko Kuhusu Utenzi wa Omar Khayyam na Tafsiri Zake.....	20
2.2.5 Maandiko Kuhusu Kulinganisha na Kulinganua Matini za Kifasihi	22
2.3 Mapengo Yaliyojitokeza Kutokana na Mapitio ya Maandiko	23
2.4 Kiunzi cha Nadharia ya Utafiti	24
2.4.1 Nadharia za Ulinganifu	24
2.4.2 Jinsi Nadharia za Ulinganifu Zilivyotumika katika Utafiti Huu.....	26
2.5 Muhtasari wa Sura ya Pili	26
SURA YA TATU	28
METHODOLOJIA YA UTAFITI	28
3.1 Utangulizi.....	28
3.2 Usanifu wa Utafiti	28
3.3 Eneo la Utafiti	28
3.4 Walengwa wa Utafiti.....	29
3.4.1 Jamii ya Watafitiwa.....	29
3.4.2 Usampulishaji na Sampuli Iliyotumika.....	29
3.5 Ukusanyaji wa Data	30
3.6 Njia na Zana za Kukusanyia Data	30
3.6.1 Mahojiano	30
3.6.2 Majadiliano ya Vikundi	31
3.6.3 Udurusu wa Maandiko	31
3.7 Mchakato wa Ukusanyaji wa Data na Udhhibiti wake	32

3.8 Uchanganuzi wa Data	32
3.9 Uzingativu wa Itikeli ya Utafiti.....	33
3.10 Uhalali na Uthabiti wa Matokeo ya Utafiti	33
3.11 Mipaka ya Utafiti	34
3.12 Changamoto Zilizojitokeza na Utatuzi Wake	34
3.13 Muhtasari wa Sura ya Tatu	35
SURA YA NNE.....	36
UWASILISHAJI NA MJADALA WA MATOKEO YA UTAFITI.....	36
4.1 Utangulizi.....	36
4.2 Jamii ya Waajemi	36
4.3 Mbinu Zilizotumika Kutafsiri <i>Utenzi wa Omar Khayyam</i>	38
4.3.1 Muhtasari wa Tafsiri za Utenzi wa Omar Khayyam.....	39
4.3.1.1 Muhtasari wa Tafsiri ya Edward FitzGerald.....	39
4.3.1.2 Muhtasari wa Tafsiri ya Shaaban Robert.....	40
4.3.2 Mbinu Walizotumia Edward FitzGerald na Shaaban Robert Kutafsiri <i>Utenzi wa Omar Khayyam</i>	42
4.3.2.1 Uzingatizi wa Umbo la Matini Chanzi.....	42
4.3.2.2 Uzingatizi wa Maudhui	46
4.3.2.3 Uzingatizi wa Utamaduni wa Jamii ya Lugha Lengwa	51
4.3.2.4 Uzingatizi wa Mazingira	56
4.4 Kufanana na Kutofautiana kwa Tafsiri Mbili za Utenzi wa Omar Khayyam.....	60
4.4.1 Kufanana kwa Tafsiri za Utenzi wa Omar Khayyam	61
4.4.1.1 Kufanana katika Mbinu za Kufanya Tafsiri.....	61
4.4.1.2 Kufanana wa Kimaudhui.....	61
4.4.1.3 Kufanana katika Mtindo (Kuzingatia Vina na Mizani).....	62
4.4.1.4 Kufanana Katika Nia ya Kutafsiria Jamii Zao	64
4.4.2 Kutofautiana kwa Tafsiri Hizi.....	65
4.4.2.1 Tofauti za Kiutamaduni.....	66
4.4.2.2 Tofauti za Kimazingira	68
4.4.2.3 Tofauti za Kiisimu.....	70
4.5 Sababu za Kuwapo kwa Mwachano wa Tafsiri Hizi za <i>Utenzi wa Omar Khayyam</i>	71

4.5.1 Ugumu wa Kutafsiri Utanzu Husika	71
4.5.2 Tofauti za Kiisimu.....	74
4.5.3 Tofauti za Kiutamaduni	75
4.5.4 Mihula Tofauti ya Nyakati	78
4.6 Muhtasari wa Sura ya Nne	79
SURA YA TANO	80
MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO	80
5.1 Utangulizi.....	80
5.2 Muhtasari wa Tasnifu.....	80
5.3 Hitimisho.....	82
5.3.1 Utoshelevu wa Nadharia Iliyotumika	82
5.3.2 Mchango Mpya wa Tasnifu	83
5.3.3 Mapendekezo kwa Tafiti Zijazo	83
MAREJELEO	85
VIAMBATISHO	89

ORODHA YA VIFUPISHO VILIVYOTUMIKA

Bi.	Bibi
Bw.	Bwana
CHAKITA	Chama cha Kiswahili Tanzania
Dkt.	Daktari
DUP	Dar es Salaam University Press
Khj	Keshatajwa hapo juu
LC	Lugha Chanzi
LL	Lugha Lengwa
MA	<i>Master of Arts</i>
MC	Matini Chanzi
ML	Matini Lengwa
Na.	Namba
Pg.	<i>Page</i>
PhD	<i>Doctor of Philosophy</i>
Prof	Profesa
Tar.	Tarehe
TATAKI	Taasisi ya Taaluma za Kiswahili
TUKI	Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili
Uk.	Ukurasa
Vol.	<i>Volume</i>
www	<i>world wide web</i>

SURA YA KWANZA

UTANGULIZI

1.1 Ufafanuzi wa Istilahi Muhimu Zilizotumika katika Utafiti Huu

Hii ni sehemu inayohusu ufafanuzi wa istilahi mbalimbali zilizotumika katika utafiti huu ili, kurahisisha uelewaji wa msomaji wa utafiti huu. Kila istilahi imetolewa maelezo ya kutosha kuifafanua ili ieleweke vizuri.

1.1.1 Tafsiri

Mwansoko (2013) anasema kuwa tafsiri ni zoezi la uhawilishaji wa mawazo katika maandishi, kutoka lugha moja hadi nyingine. Naye, Catford (1965) anasema kuwa kufasiri ni kuchukua mawazo yaliyo katika maandishi, kutoka lugha chanzi na kuweka badala yake mawazo yanayolingana kutoka katika lugha lengwa. Masamba (2000) akieleza dhana ya tafsiri, anasema kuwa ni habari iliyohamishwa kutoka lugha chanzi na kuingizwa katika lugha lengwa.

1.1.2 Mfasiri

TUKI (2000) wanasema ni mtu anayefanya tafsiri kutoka lugha moja hadi lugha nyingine. Mfasiri ni mtu yeyote anayejishughulisha na kazi za kutafsiri, ni mtu mwenye taaluma au ujuzi wa kutafsiri. Mfasiri anatakiwa awe mahiri wa lugha mbili zinazofanyiwa tafsiri kwa kujua vizuri nyanja mbalimbali za isimu ya lugha husika kama vile, fonolojia-matamshi, mofolojia-maumbo, sintaksia-maumbo na semantiki-maana. Pia, ajue utamaduni na mazingira ya lugha zote mbili anazozifanyia kazi.

1.1.3 Ulinganisho na Ulinganuzi

Ponera (2014) anasema kuwa, ulinganisho ni kitendo cha kufanya tathmini ya vitu viwili au zaidi ili kujua ubora, kufanana na kutofautiana kwavyo. Anafafanua vipengele vinavyotakiwa kuzingatiwa wakati wa kufanya ulinganisho, ambavyo ni

maana, utamaduni, upokezi, unusura, uigizaji na uathiriano. Vipengele vingine ni uwakati, mtagusano, tanzu mbalimbali, ukanda, mbinu za kibunilizi, mbinu za kimuundo, motifu na mtindo. Naye, Wamitila (2003) anafafanua kuwa, ulinganuzi ni kitendo cha kuchunguza, kuchambua na kuonesha sifa zinazotofautiana baina ya vitu (matini) viwili au zaidi.

1.1.4 Matini Chanzi

Matini chanzi ni ile matini ambayo iko katika lugha yake ya awali au lugha yake iliyoandikiwa kabla ya mchakato wa kutafsiriwa. Kwa mfano, Shaaban Robert alitafsiri *Utenzi wa Omar Khayyam* kutoka lugha ya Kiingereza. Kwa hivyo, matini hii ya Kiingereza ndiyo matini chanzi ya tafsiri hii ya Shaaban Robert.

1.1.5 Matini Lengwa

Matini lengwa ni ile matini iliyotafsiriwa kutoka lugha iliyoandikiwa. Kwa mfano, *Utenzi wa Omar Khayyam* ulio katika lugha ya Kiswahili ni matini lengwa, kwani imetafsiriwa kutoka lugha ya Kiingereza kuja lugha ya Kiswahili. Kwa hiyo, matini hii ya Kiswahili ndio matini lengwa.

1.1.6 Tafsiri Nzuri/Mbaya

Mwansoko (2013) anasema kuwa, tafsiri nzuri ni ile yenye kusema vilevile kama yasemavyo makala yaliyotafsiriwa na iwe inalingana na maandishi ya asili. Tafsiri hii ieleze mambo kama kwamba lugha iliyotumika ndiyo asili iliyotumiwa kuandika makala hayo. Tafsiri nzuri huwa na maana ya kinachokusudiwa katika maandishi yaliyotafsiriwa. Pia, inashikana maana, sentensi moja inashikana na nyingine, sehemu moja ya maelezo yanayotafsiriwa inashikamana na nyingine. Kwa upande mwingine Mwansoko (khj), anasema tafsiri ya neno kwa neno inadhoofisha maana,

inaweza kupotosha maana ya kile kinachokusudiwa kwa hakika kutafsiri neno kwa neno huifanya tafsiri iwe mbovu kabisa.

1.1.7 Matini za Kishairi

Mulokozi na Kahigi (1982) wanasema kuwa ushairi ni sanaa inayopambanuliwa kwa mpangilio maalumu wa maneno fasaha na yenye muwala, kwa lugha ya mkato, picha au sitiari au ishara na katika usemi. Aidha, ushairi hupambanuliwa kwa maandishi au mahadhi ya wimbo ili kueleza hisi fulani kuhusu maisha au maisha ya binadamu kwa njia inayogusa moyo. Kwa hiyo, matini za kishairi zinatakiwa ziwe na sifa zilizoorozeshwa hapo juu.

1.1.8 Lugha Chanzi

Lugha chanzi ni lugha iliyotumika kuandikia matini chanzi au lugha asili ya matini. Kwa mfano, tafsiri ya Kiswahili ya *Utenzi wa Omar Khayyam* ilitokana na tafsiri ya Kiingereza ya EdwardFitzGerald. Kwa hiyo, lugha ya Kiingereza ndiyo lugha chanzi ya utenzi huu. Ijapokuwa lugha chanzi kabisa ya utenzi huu ni lugha ya Kiajemi lakini kwa muktadha wa tafsiri ya Shaaban Robert ya Kiswahili, lugha ya Kiingereza ndio tunaweza kuiita lugha chanzi.

1.1.9 Lugha Lengwa

Lugha lengwa ni lugha iliyotumika kutafsiria matini chanzi au lugha tunayoitumia kufanyia tafsiri. Kwa mfano, tafsiri ya *Utenzi wa Omar Khayyam* kwa Kiswahili, lugha ya Kiswahili ndio lugha lengwa kwani ndio lugha iliyotumika kutafsiria matini chanzi ya Kiingereza. Kwa hiyo, kwa muktadha huu lugha ya Kiswahili ndio lugha lengwa.

1.1.10 Utamaduni

Ponera (2014) anasema kuwa, utamaduni ni dhana ya jumla inayobeba dhana nyinginezo kama vile matumizi ya lugha, mitazamo ya jamii husika na sanaa za kijadi. Utamaduni ni jinsi binadamu anavyoyakabili maisha katika mazingira yake hivyo, inajumuisha ujuzi, imani, sanaa, maadili, sheria, desturi na mambo mengine ambayo anajipatia kama mwanajamii. Naye, Ndulute (1973) anasema kuwa, utamaduni ni sifa maalumu ya binadamu inayomtofausha na wanyama. Utamaduni ni suala la msingi katika maisha ukihusisha yale yote yanayopokezwa katika jamii fulani, kama vile lugha inayounganisha watu wanaohusika nayo, fasihi mafungamano, ndoa, michezo, ibada, sayansi na teknolojia.

1.1.11 Itikadi

Itikadi ni mkusanyiko wa imani unaoshikiliwa na kikundi cha watu fulani. Chuachua (2011) anasema kuna aina kuu mbili za itikadi, itikadi za kisiasa na itikadi za kiepistemolojia (ni sehemu ya falsafa ambayo inahusu utafiti wa jinsi tunavyoona mambo). Itikadi ya kisiasa ni upangiliaji unaohusu mawazo ya kimaadili ni vipi nchi itaendeshwa. Itikadi za kiepistemolojia ni upangiliaji unaohusu mawazo ya kifalsafa, ulimwengu na jinsi gani watu wanapaswa kufanya maamuzi. Chuachua (khj), anasema kuwa itikadi ni mawazo fulani ambayo ni misingi ya nadharia za mfumo wa kisiasa, kiuchumi na kijamii.

1.1.12 Mila na Desturi

Mila na desturi ni taratibu, kanuni, sheria na miiko ambayo jamii imejiwekea ili kuweza kuendesha maisha yao na kujitofautisha na jamii nyingine. Tarabibu, sheria, kanuni na miiko hii inaitambulisha jamii fulani kwa jamii nyingine kiasi kwamba mambo hayo yakifanywa na jamii ambayo siyo ya mila na desturi ile watu watasema

tu kuwa mbona unafanya mambo kama jamii fulani. Kwa mfano, mila na desturi za Wasukuma ni tofauti na kabila la Waruguru.

1.1.13 Mazingira

Mazingira ni jumla ya mambo yote yanayomzunguka kiumbe katika maisha yake. Kwa hiyo, kila tunachokiona katika maisha ni mazingira yetu. Mazingira huweza kuundwa na vitu mbalimbali vyaweza kuwa vya asili kama vile misitu, milima, maziwa, mabonde, mito na bahari. Mazingira pia, yanaweza kuwa ya kutengenezwa na binadamu kama vile majengo, barabara, mabwawa na misitu. Mungai (2005) anasema kuwa, mazingira katika fasihi ni pamoja na umri, tabia za wasomaji na aina ya wasomaji wa fasihi husika.

1.1.14 Mtindo

Msokile (1991) anasema kuwa mtindo ni mchanganyiko wa mambo makubwa mawili, mambo hayo ni wazo (maudhui) la msanii linaloelezwa na jinsi wazo hilo linavyoelezwa na msanii katika uandishi wa kifasihi. Mtindo pia huwa ni tabia ya uandishi katika kipindi cha mfumo fulani wa maisha ya mtu (kutokana na wakati). Mtindo ni tabia ya mtu binafsi juu ya ufundi, umahiri na hisia za kibinafsi katika kutenda mambo yake anayokutana nayo. Hivyo, tunaweza kusema kuwa mtindo ni mbinu za kipekee kifani na kimaudhui zinazomtofautisha msanii mmoja na mwingine. Kwa mfano, namna msanii anavyotumia lugha, anavyoteua msamiati, namna anavyosimulia hadithi yake na mambo mengine.

1.1.15 Muundo

Msokile (1991) anasema muundo ni mpangilio wa kiufundi anaotumia mwandishi katika kupangilia kazi yake, ni mpangilio na mtiririko wa kazi ya fasihi kwa upande

wa visa na matukio. Kwa mfano, kuna aina mbili za muundo katika utunzi wa riwaya, muundo wa moja kwa moja na muundo rejeshi.

1.1.16 Jamii ya Watafsiriwa

Jamii ni watu walio katika eneo moja na wanaoshirikiana katika mambo mbalimbali ikiwemo lugha. Aiello (2005) anafafanua dhana ya neno jamii kuwa, ni watu wanaokaa pamojana kushirikiana kwa mambo mbalimbali. Kwa mfano, masuala ya afya, lugha elimu na ulinzi. Mambo hayo yanapowakutanisha watu hujenga kitu kinachoitwa jamii. Kwa hiyo, jamii ya watafsiriwa ni jamii ya watu wanaopokea kazi ya kigeni iliyotafsiriwa kwa lugha yao na inashabihiana na mambo yao yanayowaunganisha.

1.2 Usuli wa Tatizo la Utafiti

Tafsiri ni jambo muhimu sana katika maendeleo ya binadamu, maana pasingekuwa na tafsiri binadamu asingefikia ustaarabu alionao kwa sasa. Inasemekana kuwa ustaarabu ulienea ulimwenguni ukianzia Misri, Ugriki, Uarabuni kisha Ulaya nzima na ulimwenguni kote kwa njia ya tafsiri. Tafsiri imekuwa ikifanywa katika matini za kifasihi kama vile riwaya, tamthiliya na ushairi. Watafsiri wengi wa fasihi wamekuwa wakijikita sana katika kutafsiri riwaya na tamthiliya na utanzu wa ushairi kubaki nyuma sana katika kutafsiriwa.

Utenzi unaosadikiwa kufanyiwa tafsiri nyingi ni *Utenzi wa Omar Khayyam*. Utenzi huu uliandikwa na Omar Khayyam kwa lugha ya Kiajemi na umetafsiriwa kwa lugha zaidi ya hamsini duniani. Tafsiri ya kwanza ya utenzi huu ilikuwa ya Kiingereza ya Edward FitzGerald (1859) ambaye aliutafsiri utenzi huu pia kwa lugha ya Kilatini (Yogananda, 1920).

Kama ilivyoelezwa hapo juu kuwa utenzi huu umefanyiwa tafsiri nyingi, ni dhahiri kuwa tafsiri hizi zina tofauti kutokana na muono na mwelekeo wa kila mtafsiri. Jambo hili ndilo linaloibua hoja ya kufanyia utafiti *Utenzi wa Omar Khayyam* kulinganisha na kulinganua tafsiri za utenzi huu, ile tafsiri ya Kiingereza ya Edward FitzGerald chapa ya kwanza (1859), na tafsiri ya Kiswahili ya Shaaban Robert (1973).

Mwansoko (2013) anaeleza matatizo yanayojitokeza katika kufanya tafsiri kuwa, ni matatizo ya kitamaduni, matatizo ya kiisimu, matatizo ya kimtindo na uundaji wa maneno mapya. Pia, anatoa sifa za ziada za mtafsiri na mambo anayopaswa kuzingatia wakati wa kufanya tafsiri. Anaendelea kusema kuwa, katika matini za kifasihi kinachozingatiwa siyo taarifa (maudhui) tu, yaani maana za maneno, bali pia mpangilio wa kisanii na zana zake za kiisimu (fani). Hali hii ikizingatiwa, hufanya ufasiri wa fasihi uwe tukio la kisanaa na wala siyo la lugha au isimu. Mwandishi huyu anaenda mbali zaidi kwa kutoa aina nne za tafsiri ambazo ni, tafsiri ya neno kwa neno, tafsiri sisisi, tafsiri ya kisemantiki na tafsiri ya kimawasiliano. Mwandishi huyu, anapendekeza kuwa tafsiri ya kisemantiki na tafsiri ya kimawasiliano ndizo zitumike katika kutafsiri matini za kifasihi.

Kwa mantiki hii, ili mfasiri aweze kufasiri kwa ufanisi matini za kifasihi, ni vyema na yeye awe na kipaji cha kisanii. Aidha, kwa kuwa fasihi ni kioo cha jamii basi kufasiri kazi yoyote ya kifasihi ni lazima mfasiri afahamu vema utamaduni wa jamii inayotumia lugha chanzi pia ule unaotumia lugha lengwa ili aweze kuwianisha vema tamaduni hizo. Maelezo haya yalitupa mwanga kuweza kujua aina za tafsiri na matatizo yanayoweza kujitokeza wakati wa kufanya tafsiri. Pia, tulipata wazo kuwa mfasiri wa fasihi anatakiwa awe na kipaji cha usanii na kufahamu utamaduni wa lugha chanzi na lugha lengwa. Hata hivyo, maelezo haya ni ya jumla mno hasa

yanahusu tafsiri za matini za kifasihi kwa ujumla. Tafsiri hii anayoiongelea, inakuwa imefanyika kutoka katika lugha ya matini chanzi kwenda lugha ya matini lengwa, bila kuzibainisha matini hizo. Hapa tunabaki na maswali kichwani, je changamoto katika kutafsiri matini za kifasihi zinalingana? Na inakuwaje kama matini moja imetafsiriwa kwa lugha zaidi ya moja kama ilivyo katika *Utenzi wa Omar Khayyam*? Ndulute (1973) anasema kuwa, kulingana na mazingira, utamaduni na mtazamo wa mfasiri wa kazi husika kuna mambo ambayo mtafsiri huyu hulazimika kuyaacha na kuweka maneno yake. Jambo hili hufanya baadhi ya maudhui kutokuwa na mguso kama ilivyo katika matini chanzi ambapo huifanya tafsiri hii iwe na muonjo fulani mpya. Anamalizia kwa kusema kuwa kadri matini inavyotafsiriwa, maudhui yake huzidi kuchujuka. Kwa kuwa, tafsiri huathiriwa na mambo kama utamaduni, upokezi, uwakati na aina ya matini hizo, kwa hiyo tafsiri hizi mbili lazima ziwe zinafanana na kutofautiana kwa namna moja au nyingine. Kutokana na hali hiyo, mtafiti alisukumwa kufanya utafiti wa kulinganisha na kulinganua tafsiri hizi mbili za *Utenzi wa Omar Khayyam*. Aidha, kuchunguza sababu za kuwapo kwa mwachano kati ya tafsiri hizi mbili na kubainisha changamoto za kutafsiri matini za ushairi. Kazi hii itafungua milango ya kufanya tafiti na tafsiri, katika uga huu wa ushairi kwani bado uko nyuma sana ukilinganisha na tanzu zingine.

1.3 Tamko la Tatizo la Utafiti

Wachunguzi na wahakiki kama vile Mungai (2005) na Traore (2005) wameshughulikia suala la tafsiri katika fasihi kwa namna tofautitofauti. Kwa kiasi kikubwa, uchunguzi wao umejikita katika kutoa dhana yenyewe ya tafsiri, mbinu za kufanya tafsiri, aina za tafsiri, tafsiri bora inatakiwa iwe ya namna gani na matatizo yanayoweza kujitokeza wakati wa kufanya tafsiri.

Maelezo hayo ya wataalamu yalitudhihirishia kuwa suala la kulinganisha na kulinganua tafsiri mbili, hasa inapotokea matini chanzi imetafsiriwa kwenda matini lengwa na matini lengwa hiyo imetafsiriwa tena (tafsiri ya tafsiri), halijashughulikiwa. Swali linabaki kuwa; Kama wafasiri wametumia mbinu zilizotajwa hapo juu katika kufanya tafsiri zao, inakuwaje kwa tafsiri iliyotafsiriwa? Hivyo basi, mtafiti alisukumwa na hoja hii kufanya utafiti katika tafsiri ya *Utenzi wa Omar Khayyam* ili kulinganisha na kulinganua tafsiri mbili, ile ya Kiingereza ya Edward FitzGerald (1859) na ile ya Kiswahili ya Shaaban Robert (1973).

1.4 Malengo ya Utafiti

Utafiti huu ulikuwa na lengo la jumla moja na malengo mahsusi matatu. Malengo hayo yameainishwa hapa chini.

1.4.1 Lengo la Jumla

Kuchunguza tafsiri katika ushairi kwa kufanya ulinganisho na ulinganuzi wa tafsiri mbili za *Utenzi wa Omar Khayyam*, ile ya Kiingereza ya Edward FitzGerald na ile ya Kiswahili ya Shaaban Robert.

1.4.2 Malengo Mahsusi

- a) Kufafanua mbinu zilizotumiwa na Edward FitzGerald na Shaaban Robert kutafsiri *Utenzi wa Omar Khayyam*;
- b) Kulinganisha na kulinganua tafsiri mbili za *Utenzi wa Omar Khayyam* – ile ya Kiingereza ya Edward FitzGerald na ile ya Kiswahili ya Shaaban Robert; na
- c) Kutathmini kuwapo kwa mwachano kati ya tafsiri hizi mbili za *Utenzi wa Omar Khayyam*.

1.5 Maswali ya Utafiti

Moja, mbinu zipi zilizotumiwa na watafsiri Edward FitzGerald na Shaaban Robert kutafsiri *Utenzi wa Omar Khayyam*?

Mbili, kwa namna gani tafsiri mbili za *Utenzi wa Omar Khayyam*, ile ya Edward FitzGerald na ile ya Shaaban Robert zinafanana na kutofautiana?

Tatu, mambo yepi yaliyosababisha mwachano kati ya tafsiri hizi mbili?

1.6 Manufaa ya Utafiti

Utafiti huu unatarajiwa kuleta manufaa kwa watafiti na wasomi kama ifuatavyo:

- a) Kusaidia watafiti wengine kufanya tafiti katika tafsiri ya ushairi;
- b) Utasaidia kubainisha changamoto katika kutafsiri ushairi na namna ya kukabiliana nazo;
- c) Utahamasisha kufanyika kwa tafsiri nyingi katika utanzu huu wa ushairi maana bado uko nyuma ukilinganisha na tanzu zingine;
- d) Utasaidia kuongeza uelewa juu ya mtunzi maarufu wa mashairi Omar Khayyam; na
- e) Utasaidia kuziunganisha jamii za lugha zinazofanyiwa kazi, kwani jamii hizi zitaweza kupata maudhui yaliyomo katika *Utenzi wa Omar Khayyam*.

1.7 Muhtasari wa Sura ya Kwanza

Sura hii ya kwanza imetoa ufafanuzi wa istilahi mbalimbali zilizotumika katika utafiti huu. Sura imezungumzia usuli wa tatizo la utafiti, tamko la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti na manufaa ya utafiti. Katika usuli wa tatizo, mtafiti ameonesha jinsi tafsiri ilivyoanza na namna *Utenzi wa Omar Khayyam* ulivyo maarufu na ulivyotafsiriwa kwa lugha nyingi. Aidha, kumezungumziwa tafsiri mbili za utenzi huo ile ya Edward FitzGerald na ile ya Shaaban Robert. Pia, kumeainishwa malengo na maswali ya utafiti pamoja na manufaa ya utafiti huu.

SURA YA PILI

MAPITIO YA MAANDIKO NA KIUNZI CHA NADHARIA

2.1 Utangulizi

Katika sura hii tumezungumzia mapitio ya maandiko kuhusu umuhimu na maendeleo ya tafsiri ulimwenguni. Maandiko yaliyoshughulikiwa ni kuhusu tafsiri katika fasihi, maandiko kuhusu tafsiri katika ushairi na changamoto zake na maandiko kuhusu *Utenzi wa Omar Khayyam* na tafsiri zake. Aidha maandiko mengine ni kuhusu kulinganisha na kulinganua matini za kifasihi na kisha tukaangalia mapengo yaliyojitokeza kutokana na mapitio ya maandiko hayo. Pia, kumeangaliwa kiunzi cha nadharia ya utafiti na jinsi nadharia hii ilivyotumika katika utafiti huu.

2.2 Mapitio ya Maandiko

Makundi ya maandiko yaliyopitiwa yalijumuisha maandiko kuhusu maendeleo ya tafsiri ulimwenguni, maandiko kuhusu tafsiri katika fasihi na maandiko kuhusu *Utenzi wa Omar Khayyam* na tafsiri zake. Aidha, maandiko yanayohusu mbinu za kulinganisha na kulinganua matini za kifasihi yaliangaliwakisha, kubaini mapengo yaliyopo yaliyohitajika kuzibwa na utafiti huu.

2.2.1 Maandiko Kuhusu Umuhimu na Maendeleo ya Tafsiri Ulimwenguni

Mundy (2001) akiongelea taaluma ya tafsiri anasema kuwa taaluma hii haiwezi kujitegemea peke yake. Mtaalamu huyu, anaifananisha taaluma hii na mwili wa binadamu, ambapo kiungo kimoja pekee hakiwezi kufanya kazi peke yake. Hivyo basi, anasema taaluma hii lazima iende sambamba na taaluma kama vile; ukalimani, isimu linganishi, isimu jamii, isimu amali na nyinginezo. Maelezo ya mtaalamu huyu yalitusaiaidha kujua umuhimu wa tafsiri na namna tafsiri inavyoweza kuchanagamana na taaluma nyingine. Ngugi (2013) anaona tafsiri huwa inaanza pale

tu binadamu anapozaliwa, kile kitendo cha kulia, kucheka na matendo mengine anayofanya mtoto na mama yake kuyatafsiri kama njaa au furaha. Ngugi anaiona hiyo ni tafsiri ya mwanzo kabisa katika maisha ya binadamu. Mwandishi huyu anasema:

Nimekuwa nikiishi katika tafsiri daima, kwanza tafsiri yangu mwenyewe nilipoonesha uhusiano wangu hai na dunia inayonizunguka, njaa, kiu, maumivu, ghasia, matakwa, kwa kilio cha kuendelea (kwa upande mmoja) na furaha, kutosheka na sherehe na kicheko, ambavyo kwavyo watu hususan mama yangu alichukua hatua ya kunitimizia matakwa yangu. Hii ilikuwa tafsiri ya dunia ndani na kandokando yangu kwa kupitia sauti ambazo nilikuwa nikizifanya (uk 30).

Mtaalamu huyu anaiona tafsiri katika hatua ya mwanzo kabisa ya maisha ya binadamu baada ya kuzaliwa na baadae alipoanza kuona, kusikia, kugusa na kuonja. Anasema, jambo la tafsiri liliendelea kwa mama kutoa tafsiri kwa kila alichokiona, kukisikia, kukigusa na au kukionja kwa kutumia lugha ya mama. Mwandishi huyu anaendelea kueleza kuwa, baada ya kuijua lugha ya mama, na umri wa mtu kuanza masomo hulazimika kukutana na lugha ya pili hivyo, zoezi la tafsiri huendelea. Kwa maelezo ya mtaalamu huyu, mtu anapoanza kujifunza lugha ya pili hufanya tafsiri kwa kurejelea lugha yake ya mama ambayo yeye anaiita tafsiri ya akilini. Mwandishi huyu anasema:

Katika mwaka wangu wa tatu shuleni, nilianza kujifunza Kiswahili na Kiingereza. Ili kuzielewa lugha hizo vizuri niliendelea kurejelea kwenye lugha mama, maandiko yote yaliyo katika lugha isiyo lugha mama. Maandiko yote yaliyo katika lugha isiyo lugha chanzi au lugha chanzi ya makuzi ya mtu kwa kiasi kikubwa ni tafsiri ya akilini (uk 31).

Kutokana na maelezo haya, mwandishi huyu anaiona tafsiri inaanza tu pale mtu anapozaliwa, kuanza kujitambua hadi anapokuwa mtu mzima. Hivyo, tafsiri kwake ipo katika maisha yote ya binadamu. Maelezo hayo yalitusaidia kujua umuhimu wa tafsiri na namna mchakato wa tafsiri unavyofanyika akilini mwa mtu, kwa kurejelea lugha mama. Kwa hiyo, kwa maoni yake lugha mama huendelea kurejelewa wakati

wa kutafsiri lugha ya pili. Hata hivyo, tunabaki na swali inakuwaje kama tafsiri imetafsiriwa tena, na kama kila mmoja atarejelea lugha yake mama katika kutafsiri?

Mwansoko (2013) anasema kuwa tafsiri ndilo daraja linalounganisha jamii mbalimbali za watu wanaotumia lugha zinazotofautiana. Anaendelea kueleza kuwa tafsiri ni njia ya mawasiliano, nyenzo ya kueneza utamaduni kutoka jamii moja kwenda nyingine, ni mbinu mojawapo ya kujifunza lugha za kigeni na ni kiliwazo cha nafsi ya mtafsiri. Maelezo yake yanaonesha kuwa maingiliano ya kijamii tunayoyaona sasa na dunia kuwa kama kijiji, mambo ya utandawazi na soko huria vyote vimejengwa katika daraja la tafsiri. Bila tafsiri vitu hivi visingefikiwa kwa urahisi kama ilivyo sasa. Kwa maana hiyo basi, tafsiri inatufanya kuchangamana na jamii nyingine kwa urahisi. Jambo hili alilolijadili mwandishi huyu lilitusaidia kutambua manufaa ya tafsiri miongoni mwa jamii mbili zinazofanyiwa tafsiri.

Wataalamu wengi wanakubaliana kuwa kiini cha maendeleo ulimwenguni kilisababishwa na tafsiri. Nchi ya Misri ilikuwa ya mwanzo kustaarabika. Wagriki walipokuja Misri walichukua maarifa na ustaarabu wa Wamisri na kwenda kuutafsiri kwao, jambo lililosababisha Ulaya nzima kustaarabika. Kwa maana hiyo basi, tamaduni nyingi ulimwenguni zimeweza kupiga hatua za kimaendeleo kutokana na ubadilishanaji wa maarifa miongoni mwa jamii mbalimbali kupitia tafsiri. Kelly (1979) anasema kufaulu kwa himaya ya Roma hadi kufikia ustawi wa taaluma za kimataifa katika mambo ya biashara na utawala kulifanikishwa na tafsiri. Utamaduni wa Kirumi uliathiriwa na ule wa Kiyunani kupitia tafsiri. Pia, karne ya 19 wakati wakoloni wanaingia barani Afrika walitumia sana nyenzo ya tafsiri, kwa kuanza na dini na ustaarabu wao wa kimagharibi. Baadhi ya kazi zinazohusiana na maandiko matakatifu zilitafsiriwa kwa lugha za Kiafrika na lugha za Kienyeji. Hii iliwasaidia kuchangamana kwa urahisi na jamii za wenyeji.

2.2.2 Maandiko Kuhusu Tafsiri Katika Fasihi

Mshindo (2010) akizungumzia tafsiri za matini za kazi za kifasihi anasema kuwa, kufasiri kazi za fasihi (riwaya, hadithi fupi, michezo na ushairi) inachukuliwa kuwa ni kufanya kazi ya kubuni fasihi kama alivyofanya mwandishi wa awali. Jambo ambalo anasema siyo sahihi kwani kila mmoja hufanya kazi yake kwa wakati wake, kwa madhumuni yake na kwa ajili ya walengwa wake. Katika kutafsiri matini za kifasihi hasa riwaya, anaona kuna tofauti na kutafsiri matini za kisayansi.

Mwandishi anasema:

Kufasiri riwaya ni tofauti na kufasiri sayansi. Sayansi inajishughulisha na vilimwengu, na tafsiri za kitaalamu zinazoweza kupokewa vyema na wasomi wenye maslahi nazo. Matukio kama riwaya ni ya kufikirika-nusu, kwa vile yamesanifiwa ili kuvutia hisia za jamii (uk 231).

Maelezo hayo yalitusaikia kupata mwanga juu ya tofauti iliyopo kati ya kutafsirimatini za kisayansi na zile za kifasihi, mambo ambayo yalitusaikia katika utafiti wetu kujua utofauti uliopo kati ya tafsiri za kisayansi na tafsiri za kifasihi hasa ushairi.

Mshindo (khj), akielezea kuhusu tafsiri katika fasihi, anakiri kuwa siyo rahisi kupata tafsiri timilifu isipokuwa kinachotakiwa ni kupata tafsiri toshelevu ambayo inakidhi matakwa ya mfasiri na msomaji kwa maana ya ujumbe uliokusudiwa kufika kwa mlengwa. Mshindo (khj) anazungumzia mambo manne ambayo mfasiri hufanya kazi ya kufasiri huku akiwa anayazingatia. Kwanza kuwa, kufasiri ni sayansi ambayo inajumuisha maarifa na uthibitishaji wa taarifa na lugha ambayo inazieleza. Pili kuwa, kufasiri ni stadi ambayo inahitaji kutumia lugha inayofaa na matumizi yanayokubalika. Tatu kuwa, kufasiri ni sanaa ambayo hupambanua maandishi bora na maandishi mabaya na nne ni kuwa, kufasiri ni suala la matamano. Maelezo hayo yalitufanya tujue mambo yanayotakiwa kuzingatiwa na mfasiri anapokuwa anatafsiri

kazi yoyote ile ya kifasihi. Mambo hayo yalitusaidia katika utafiti wetu kujua wafasiri wa *Utenzi wa Omar Khayyam* kama walizingatia vipengele hivyo katika kufanya tafsiri zao ili kujua ulinganifu na utofauti kati ya tafsiri hizi mbili.

Mwansoko (2013) anatoa mbinu za kufanya tafsiri kwa kueleza mbinu nne. Mbinu hizo ni tafsiri ya neno kwa neno, tafsiri sisisi, tafsiri ya kisemantiki na tafsiri ya mawasiliano. Anaongeza kusema kuwa, katika mbinu hizi nne, ni mbinu mbili tu ambazo zinaweza kukidhi haja ya kutafsiri matini za kifasihi ambazo ni tafsiri ya kisemantiki na tafsiri ya kimawasiliano. Hii ni kwa sababu, hukidhi malengo makuu ya tafsiri ambayo ni kutoa taarifa zilizosahihi na kuzingatia iktisadi ya lugha. Maelezo hayo yalitusaidia kujua mbinu nzuri za kutumia unapotaka kufanya tafsiri za matini za kifasihi, ijapokuwa mwandishi huyu amependekeza mbinu hizi kutumika katika kutafsiri matini zote za kifasihi. Swali lililobaki la kujiuliza ni je, mbinu hizi zinaweza kufaa kwa namna sawa katika tanzu zote za kifasihi yaani riwaya, tamthiliya na ushairi? Swali lingine tulilojiuliza inakuwaje kama mtu ametafsiri matini kutoka katika matini tafsiri?

Traore (2005) akizungumzia tafsiri za riwaya za kigeni kwa Kiswahili nchini Tanzania akigusia tafsiri ya kitabu cha *Shamba la Wanyama*, anataja mbinu alizotumia mfasiri katika kufasiri. Mbinu hizo ni kubadili mazingira na kuyafanya ya kienyeji kulingana na hadhira yake na alibadili majina ya wahusika ili waendane na mazingira ya hadhira lengwa. Aidha alitumia mbinu ya kuondoa maneno ya kitamaduni ya Kiingereza na kuweka badala yake maneno ya Kiswahili na mbinu ya kuandika baadhi ya aya upya.

Maelezo hayo yalitusaidia katika utafiti wetu kujua kama mbinu hizi zilitumiwa na watafsiri Edward FitzGerald na Shaaban Robert ili kuweza kulinganisha na

kulinganua tafsiri hizi mbili za *Utenzi wa Omar Khayyam* ile ya Kiingereza na ile ya Kiswahili. Hii ni kwa sababu, mazingira na tamaduni ya lugha hizi ni tofauti.

Mungai (2005) akiwanukuu Puurtinen (1998), Davies (2008), na Oittinen (2008), anasema kuwa makala yaliyotafsiriwa mara nyingi huelekea kuwa tofauti na makala asilia kwa njia mbalimbali. Tafsiri yoyote ile huhitaji kuzingatia na kutilia maanani elementi za kimazingira kuhusu wasomaji kabla ya kuamua ni mchakato gani utakaofuatwa katika kutafsiri. Mazingira haya ni pamoja na umri, tabia za wasomaji na aina za wasomaji. Mungai (khj), anaendelea kueleza kuwa mfasiri anahitajika kuwa mjuzi wa lugha zinazohusika, ili aweze kuifasiri maana iliyoko katika matini asilia na kuiunda upya katika matini lengwa. Isitoshe, kipawa cha usanii ni muhimu katika kumsaidia mfasiri kutumia lugha kibunifu ili iwe na mvuto kwa walengwa wake. Mfasiri asipokuwa na ujuzi huu, tafsiri yake huwa kavu na hudhihirisha udhaifu wa aina fulani na kinachoshauriwa asitie chumvi kupita kiasi. Maelezo hayo yaliibua hamu ya kutaka kuchunguza tafsiri hizi mbili za *Utenzi wa Omar Khayyam* ili kujua kama watafsiri hawa hawakutia chumvi. Pia, kuangalia kama ubunifu waliotumia katika kufanya tafsiri haukupotoa utamu wa matini asilia ile ya kiajemi, kwani kama mtaalamu huyu anavyosema, kadri makala inavyotafsiriwa huelekea kuwa tofauti na makala asilia.

2.2.3 Maandiko Kuhusu Tafsiri Katika Ushairi na Changamoto Zake

Maandiko haya yanayohusu tafsiri katika ushairi na changamoto zake, yamewekwa kipekee kwani wataalamu wengi wanakubaliana kuwa changamoto za kutafsiri ushairi ni tofauti na changamoto za kutafsiri matini nyingine za kifasihi kama vile riwaya na tamthiliya. Ruhumbika (1983) akizungumzia lugha ya tafsiri za fasihi, anasema kuhusiana na ushairi kuwa, una changamoto kubwa kutokana na kuwa na

ulazima wa mpangilio wa maneno, sarufi, kufupisha au kurefusha baadhi ya maneno ili kupata urari wa vina na mizani. Mwandishi huyu anasema:

Lugha ya fasihi kwa upande mwingine, mara nyingine hubidi iwe kinyume cha hiyo lugha wazi na sahihi. Mafumbo, methali na misemo ya kila aina yenye maana zilizofichika ndiyo ya lazima kwenye fasihi fulani. Na katika ushairi mara nyingi mpangilio wa maneno unaokiuka miiko ya sarufi huwa ni lazima na mara nyingine huwa ni lazima kufupisha au kurefusha maneno ili kupata urari fulani wa mizani (uk 94).

Maelezo hayo yalituonesha changamoto zilizopo katika kutafsiri matini za kishairi. Changamoto hizo ni tofauti na unapokuwa unatafsiri tanzu zingine, maana lugha ya kishairi kila neno hutakiwa kutazamwa kwa uzito wake. Pia, mpangilio wa maneno ni kitu muhimu sana katika kufanya tafsiri ya ushairi si kama katika tanzu zingine.

Newmark (1988) anasema kuwa ushairi ndiyo utanzu wa fasihi ulio mgumu zaidi kufasirika. Hii ni kwa sababu, kila neno katika ushairi lina maana na ushairi una mshindilio mkubwa wa mawazo. Naye, Mwansoko (2013) akishadidia hili anasema kuwa, katika ushairi neno na mstari licha ya kubeba maana lakini, lina umuhimu mkubwa sana katika utanzu huu kuliko tanzu nyingine. Hii ni kwa sababu, licha ya kubeba maana za kawaida, neno pia hubeba sauti na milio kwa namna ya kimpangilio tofauti na tanzu zingine. Mwandishi akilielezea hili anasema:

Katika kufasiri ushairi ni muhimu kila neno katika mstari na kila mstari katika ubeti vishughulikiwe na kuzingatiwa kwa uzito uleule. Halikadharika inasisitizwa kwamba ni vema tafsiri ya ushairi ihifadhiumbo la matini asilia. Hii ina maana kwamba mfasiri hana budi ajitahidi kuwa na idadi ileile ya mathalani, maneno, sauti, milio, sitiari, mistari na hata vistari, nukta. n.k katika tafsiri yake kama ilivyo katika matinichanzi.(uk 43-44).

Maelezo hayo yalitusaidia kujua kuwa, unapokuwa unatafsiri ushairi uzingativu na umakini unatakiwa kuwa mkubwa sana tofauti na unapokuwa unatafsiri riwaya au tamthiliya. Hii ni kwa sababu, katika ushairi kila neno lina maana na uzito wa kipekee tofauti na tanzu zingine. Jambo hili lilitusaidia kujua kama mambo hayo

yalizingatiwa na wafasiri katika kufanya tafsiri ya *Utenzi wa Omar Khayyam* wakati wa kulinganisha na kulinganua tafsiri hizi.

Makacha (2013) akiongelea kuhusu kufasiri ushairi kuwa, wafasiri wengi wanakubaliana katika jambo moja kuwa, kufasiri ushairi ni jambo gumu na tena lisilowezekana. Anaendelea kueleza kuwa mtaalamu Popovic (1970) ndiye aliyeonesha mwanga kuwa zoezi hili la kutafsiri ushairi linawezekana. Pamoja na hayo, Makacha (khj) anakiri kuwa kufasiri ushairi ni kazi ngumu, ukilinganisha na tanzu zingine kwa sababu ya fani yake itumikayo kwa uzito katika kuyasawiri maudhui. Mwandishi anasema:

Katika ushairi fanani huelezea hisia zake kwa uzito, kwa mguso na kwa muhtasari zaidi kuliko katika tanzu nyingine. Athari ya maudhui yaliyo katika umbo la kishairi huwa kubwa zaidi kuliko tanzu nyingine (uk 59).

Maelezo haya yalituonesha kuwa kufasiri ushairi ni kazi ngumu ukilinganisha na tanzu zingine, kwani mfasiri wa ushairi anatakiwa kuzingatia kila neno na bila kusahau umbo la ushairi husika katika kufasiri kwake. Mtaalamu huyu anaendelea kueleza kuwa, kuna changamoto nyingi katika kutafsiri ushairi, lakini anapendekeza shairi litafsiriwe kishairi ili kupunguza dosari katika tafsiri hiyo. Mwandishi anasema:

Kutafsiri shairi kishairi kunampa fursa mshairi kutumia tamathali za semi, kukiuka utaratibu wa kawaida. Utaratibu wa kawaida wa mfuatano wa maneno katika tungo na kutumia ishara, picha na taswira. Kwa kufasiri shairi kishairi mfasiri anakuwa ameyapa maudhui aliyoyatafsiri ladha yake ya kisanaa (uk 61).

Maelezo haya yalitupa ugumu mwingine wa kutafsiri ushairi, kwani anayetakiwa kutafsiri ushairi ni lazima awe mshairi tena, alitafsiri shairi kwa kulitunga upya. Jambo hili linaleta mkanganyiko wa kufanya tafsiri katika ushairi hasa inapotokea shairi limetafsiriwa kwa zaidi ya lugha moja kama ilivyo katika *Utenzi wa Omar*

Khayyam. Hata hivyo, mwandishi huyu anakiri kuwa pamoja na kulitunga shairi upya kamwe, tafsiri hiyo haiwezi kuwa sawa kwa asilimia miamoja kwa sababu ya utofauti wa lugha chanzi na lugha lengwa kiisimu, mtindo, itikadi, mazingira, mila, utamaduni na mitazamo yao ya maisha. Mwandishi anasema:

Siyo rahisi kwa tafsiri kuwa sawa kabisa na matini chanzi, tofauti za kiisimu, kiutamaduni, kihistoria na kimazingira baina ya lugha hufanya iwe vigumu kufasiri mawazo ya lugha moja katika lugha nyingine bila kupoteza, kupotosha au kubadili maana kwa kiwango fulani. Hii inapelekea tafsiri zote kuwa na upungufu fulani (uk 67).

Maelezo hayo yalituwekea wazi changamoto za kufanya tafsiri kuwa, kuna changamoto za tofauti za kiisimu, kiutamaduni, kihistoria na kimazingira baina ya lugha chanzi na lugha lengwa. Changamoto hizo hufanya tafsiri iwe na mapungufu fulani na isijitosheleze. Mshindo (2010) akizungumzia kuhusiana na changamoto za kufasiri matini za kishairi, anasema kuwa kunahitaji mazingatio makubwa sana. Tena yeye, anaita mazingatio maalumu kwani kuna utofauti mkubwa linapokuja sualala kutafsiri ushairi, kwani baadhi ya wataalamu watafsiri waliwahi kutamka kabisa kuwa tafsiri ya ushairi haiwezekani. Mwandishi huyu anasisitiza mambo ya kuzingatia wakati mtu anapotafsiri ushairi; anasema:

Katika kufasiri kazi za ushairi, mfasiri anapaswa kuelewa kuwa ushairi unavipengele maalumu vya kiuandishi ambavyo mtunzi huvitumia katika ubunifu wake ili kuifanya kazi yake ivutie kwa wasomaji na wasikilizaji wake. Kwa hiyo mfasiri wa ushairi anapaswa kuchunguza kwa makini sana vipengele maalumu vilivyotumiwa na mwandishi wa kazi ya ushairi kwa madhumuni ya kuviaksi vipengele hivyo katika tafsiri (uk 234).

Maelezo hayo yalituonesha umakini unaohitajika kwa mfasiri anapokuwa anatafsiri ushairi kwani, ushairi una vipengele vingi vinavyotakiwa kuzingatiwa tofauti na tanzu zingine hivyo, anaondoa uwezekano wa ushairi kutotafsirika kama wataalamu wenginewalivyodai.

Ombaga (1986) anaeleza kuwa katika tafsiriya fasihi ya Kiswahili, utanzu unaokabiliwa na changamoto zaidi katika kufasiriwa ni utanzu wa ushairi. Changamoto hizi hutokana na lugha yake kuwa ngumu na ya kisanaa, kutumia maneno ya mkato na machache, matumizi ya lugha ya kitaswira, muundo na mtindo wake kuwa tofauti na tanzu zingine, mfano urari wa vina na mizani. Hivi ni moja ya vipengele muhimu katika ushairi na ni vipengele ambavyo huleta changamoto katika kufasiri mashairi. Maelezo ya mtaalamu huyu yalitusaidia kuzitambua changamoto katika kufasiri ushairi, kitu ambacho tulikizingatia wakati wa kulinganisha na kulinganua tafsiri za *Utenzi wa Omar Khayyam*. Pamoja na kuzionesha changamoto hizo katika kufanya tafsiri ya ushairi, lakini bado anaacha maswali ya kujiuliza kama matini ya ushairi imefasiriwa kwa zaidi ya lugha moja, je changamoto atakazokutana nazo mtafsiri wa tafsiri zitakuwa zilezile?

2.2.4 Maandiko Kuhusu Utenzi wa Omar Khayyam na Tafsiri Zake

Omar Khayyam alikuwa ni mtunzi maarufu wa mashairi. Miongoni mwa kazi zake mashuhuri ni utenzi wake ujulikanao kama *Utenzi wa Omar Khayyam*. Utenzi huu ni miongoni mwa tenzi maarufu duniani na unatokana na mashairi yake yajulikanayo kama mashairi ya *Rubaiyat* (unne), ikiwa na maana mashairi yenye mishororo minne kwa kila ubeti. Utenzi huu uliandikwa na Omar Khayyam kwa lugha ya Kiajemi na unasadika kufanyiwa tafsiri nyingi.

Yogananda (1920) akiuelezea utenzi huu na mtunzi wake anasema kuwa ni miongoni mwa tenzi maarufu duniani na unaotokana na mashairi ya Omar Khayyam yajulikanavyo kama mashairi ya *rubaiyat* (unne), kwa maana ya mashairi yenye mishororo minne kila ubeti. Naye, McCarthy (1889) akiongelea tafsiri za utenzi huu anasema umefasiriwa kwa zaidi ya lugha hamsini duniani, ikiwemo Kijerumani, Kifaransa, Kirusi, Kiswidishi, Kipolishi, Kiingereza na lugha nyinginezo. Tafsiri ya

kwanza ya utenzi huu ilikuwa ya Kiingereza ya Edward FitzGerald mwaka 1859 ambayo imepigwa chapa mara tano. Chapa ya kwanza 1859, chapa ya pili 1868. chapa ya tatu 1872, chapa ya nne 1879 na chapa ya tano 1889. Pia, Edward FitzGerald alitafsiri utenzi huu kwa lugha ya Kilatini.

Mojawapo ya tafsiri ya Kiingereza ya Utenzi huu iliyo maarufu ni ya Paramahansa Yogananda (1920), ambaye alikuwa ni mfasiri wa masuala ya kiroho. Yeye anaibeza tafsiri ya Edward FitzGerald kuwa haikuzingatia mguso wa kiroho kama wa Omar Khayyam. Hii ni kwa sababu (kwa maelezo ya Yogananda), Omar Khayyam alikuwa Sheikh na alikuwa mcha Mungu wa kutiliwa mfano. Kwa hiyo, kile alichokiandika kilikuwa cha kiroho ni vema kikatafsiriwa kiroho badala ya kuyaona mashiri haya kuwa ni ya kawaida kama alivyofanya Edward FitzGerald. Omar Khayyam alikuwa mtunzi mashuhuri wa mashairi wa karne yake na inasadikiwa alitunga mashairi kiasi cha 1200 (Nafsi, 2006) hata kuitwa Shakespeare wa bara la Arabuni kwa maandiko yake. Omar Khayyam alizaliwa Nishapur Mei 1040 huko Uajemi. Baba yake aliitwa Ibrahim, inadhaniwa alikuwa fundi mahema (Khayyam maana yake fundi mahema). Omar Khayyam alikuwa pia mtaalamu wa Hisabati, Falaki (utaalamu wa kubashiri mambo mbalimbali kwa kutumia nyota) na Falsafa. Alifariki mwaka 1131.

Chuachua (2011), akizungumzia wasifu wa Shaaban Robert anasema kuwa, alizaliwa 01/09/1909 katika mtaa wa Vibambani, kijiji cha Machui mkoani Tanga. Baba yake anaitwa Suleiman Ufukwe Robert na mama yake anaitwa Bi. Mwanamwema. Shaaban Robert ni mtunzi maarufu wa riwaya na ushairi. Pamoja na kuwa bingwa wa utunzi wa mashairi na nathari, pia ana mchango mkubwa katika taaluma ya tafsiri kwa kuandika kitabu cha *Kielelezo cha Fasihi* ambamo alitoa mawazo yenye kujenga kuhusiana na tafsiri. Alitafsiri kitabu chake cha *Almasi za*

Afrika kwa lugha ya Kiingereza pamoja na kutafsiri *Utenzi wa Omar Khayyam* (1973) kutoka tafsiri ya Kiingereza ya Edward FitzGerald chapa ya kwanza. Alifariki dunia 22/06/1962. Taarifa hizi zilitusaidia kumfahamu Shaaban Robert ili kuona na kuiamini tafsiri yake aliyoifanya.

2.2.5 Maandiko Kuhusu Kulinganisha na Kulinganua Matini za Kifasihi

Remark (1971) anafasili fasihi linganishi kama, uwanja wa kifasihi unaohusika na uchanganuzi na mahusiano ya kifasihi nje ya mipaka ya nchi moja, pia kati ya fasihi na fani nyinginezo. Naye, Msokile (1996) akizungumzia ulinganishi na ulinganuo wa hadithi fupi andishi na riwaya, anasema ulinganisho uliopo kati ya hadithi fupi na riwaya za Kiswahili kuwa ni urefu, uchangamano, wahusika, dhamira na mandhari. Mawazo hayo yalitupa mwanga, vitu vya kuzingatia wakati wa kulinganisha fasihi, ijapokuwa bado yanaacha maswali hasa tunapolinganisha na kulinganua tafsiri za ushairi.

Wamitila (2003) akielezea dhana ya ulinganisho wa fasihi kuwa ni mbinu ya kuchunguza, kuchambua na kueleza sifa za mfanano zilizopo katika matini ya fasihi. Pia, ulinganuzi ni kuchunguza, kuchambua na kuonesha sifa zinazotofautiana baina ya matini mbili au zaidi za kifasihi. Mawazo haya yanaungwa mkono na Dominique (2012) anaposema kuwa, fasihi linganishi ni taaluma inayohusiana na fasihi, pamoja na maelezo ya tamaduni kupitia fasihi. Tamaduni hizi lazima ziwe zinavuka mipaka yake.

Basnett (1993), akielezea fasihi linganishi, kwa kuangalia mawanda ambayo mtu anatakiwa kuyazingatia ikiwemo ulinganisho wa kitamaduni, mazingira na maeneo ya kijiografia ili kutoa ulinganisho unaofaa. Mawazo hayo kwa kiasi fulani yanaungwa mkono na Palmer (1996) ambaye anasisitiza kuwa, wakati unafanya

ulinganisho wa fasihi kitu cha muhimu na cha msingi kuzingatiwa ni utamaduni wa jamii hizi mbili.

Ponera (2014) anasema kuwa kulinganisha ni kitendo cha kufanya tathmini ya vitu viwili au zaidi ili, kujua ubora, kufanana, na kutofautiana kwavyo. Anaeleza kuwa katika kulinganisha unatakiwa kuwa na vitu vitatu yaani; maarifa juu ya ujuzi juu ya vilinganishwavyo, kuwapo kwa vitu viwili au zaidi vinavyolinganishwa na kuwapo kwa kigezo au vigezo maalumu vya kulinganishia.

Ponera (khj) anafafanua vipengele vya ulinganisho vinavyotakiwa kuzingatiwa wakati mtu anafanya ulinganisho wowote wa kazi za kifasihi. Mwandishi huyu anasisitiza sana kuzingatia vipengele hivi wakati wa kufanya ulinganisho wa kifasihi. Akivitaja vipengele hivyo anasema:

Mwana-Fasihi linganishi anaweza kufanya ulinganisho kwa kujikita katika vipengele vingi vinavyojitokeza katika kazi ya kifasihi. Baadhi yavyo ni hivi vifuatavyo: Maana, utamaduni, upokezi, unusura, uigizaji na uathiriano, uwakati, mtagusano, tanzu mbalimbali, ukanda, mbinu za kibunilizi, mbinu za kimuundo, motifu na mtindo (uk 53-54).

Waandishi hawa walitupa mwanga ambao ulitusaidia kujua dhana ya ulinganisho na ulinganuzi pia, kujua vigezo vinavyotumika katika kulinganisha na kulinganua matini za kifasihi. Lakini, wataalamu hawa hawakuzungumzia ulinganisho wa tafsiri mbili hasa ulinganisho katika matini za kishairi kama vigezo hivyo tunaweza kuvitumia endapo tafsiri imetafsiriwa tena. Kwa hiyo, tunabaki na maswali kama vipengele hivi tunaweza kuvitumia pia katika kulinganisha na kulinganua tafsiri mbili katika ushairi kama ilivyo katika *Utenzi wa Omar Khayyam*.

2.3 Mapengo Yaliyojitokeza Kutokana na Mapitio ya Maandiko

Baada ya kufanya mapitio ya maandiko mbalimbali, tuliona kuwa maandiko hayo yameishia katika kutoa mawazo ya jumla kuhusu tafsiri. Wataalamu hawa wametoa

mawazo juu ya namna ya kufanya tafsiri na mambo ya kuzingatia wakati wa kufanya tafsiri. Mambo waliyoyajadili ni kutafsiri shairi kwa kuunda shairi upya, pamoja na kufasiri kwa kuzingatia mazingira ya hadhira lengwa.

Mambo hayo waliyoyajadili wataalamu hawa bado yanaacha maswali ya kujiuliza juu ya tafsiri iliyotafsiriwa (tafsiri ya tafsiri). Maswali hayani; kama shairi litatafsiriwa kwa kuunda shairi upya na kuzingatia mazingira ya hadhira lengwa je, matini hii ya tatu itakuwa imepotoka kwa kiasi gani kutoka matini asilia? Swali lingine la kujiuliza je, hizi tafsiri mbili zitakuwa zinafanana na kutofautiana kwa kiasi gani? Maswali haya hayajibiwa na wataalamu hawa. Hivyo, utafiti huu ulikusudia kuchunguza tafsiri mbili za *Utenzi wa Omar Khayyam*, ile ya Kiingereza ya Edward FitzGerald na ile ya Kiswahili ya Shaaban Robert iliyotokana na ile ya Kiingereza toleo la kwanza, ili kujibu maswali haya.

2.4 Kiunzi cha Nadharia ya Utafiti

Sehemu hii inafafanua kwa ufupi nadharia iliyotumiwa na mtafiti katika utafiti wake, kwa kutaja nguzo za nadharia hii na waasisi wa nadharia husika. Pia, kuna maelezo ya jinsi nadharia hii ilivyotumiwa na mtafiti kama nguzo ya kusimamia wakati wa mchakato wa utafiti.

2.4.1 Nadharia za Ulinganifu

Jilala na wenzake (2016) wanaeleza kuwa nadharia nyingi huitazama tafsiri kama tendo la kiisimu, ambalo hushughulika na mambo ya kiisimu katika lugha. Hata hivyo, miaka ya hivi karibuni wataalamu wengi wameanza kuiangalia tafsiri katika mawanda mapana ya kiutamaduni na mawasiliano, jambo ambalo lilisababisha kuibuka kwa nadharia za ulinganifu katika tafsiri.

Nadharia hizi za ulinganifu ziko katika makundi matatu, ambayo nayo yanajisimamia kama nadharia. Watetezi wa nadharia hizi ni Nida (1964), Catford (1965), Nida na Taber (1969) na Reiss (1971/2000). Nadharia hizi zinasisitiza mtekenyo sawa wa ujumbe kwa hadhira. Hii ina maana kuwa, hadhira ipate muonjo sawa wa matini iliyotafsiriwa kama ilivyo katika matini chanzi. Jambo la msingi katika nadharia hizi ni kufikia usambamba fulani baina ya lugha chanzi na lugha lengwa.

Makundi ya nadharia hizi ni nadharia ya ulinganifu wa kimuundo, nadharia ya ulinganifu wa kidhima na nadharia ya ulinganifu wa aina za matini. Nadharia ya ulinganifu wa kimuundo, ni mkabala wa kimapokeo unaosisitiza matini kutafsiriwa kwa tafsiri sisisi au tafsiri ya neno kwa neno. Nadharia ya ulinganifu wa kidhima (usawe), ilianzishwa na Eugen A. Nida katika miaka ya 1960. Hii ndiyo nadharia ya kwanza ya tafsiri ya kimawasiliano, iliyolenga kuondoa tofauti zilizokuwepo baina ya utamaduni na isimu katika tafsiri. Nadharia hii inasisitiza kanuni ya athari sawa ambapo uhusiano baina ya hadhira na ujumbe katika lugha lengwa ulingane na hadhira na ujumbe katika lugha chanzi. Nadharia hii inasisitiza kuwepo kwa mtekenyo sawa kati ya matini chanzi na matini lengwa.

Makaryk (1993) anaweka wazi kuhusu tafsiri ya ulinganifu wa kidhima kwamba, tafsiri isionekane kuwa tafsiri, bali kazi asilia katika lugha lengwa. Kwa hiyo, anasisitiza mfasiri kutafuta visawe ulinganifu katika lugha lengwa ambavyo ni vya karibu zaidi na ujumbe wa lugha chanzi.

Nadharia nyingine ni ya ulinganifu wa aina za matini. Hii inapendekezwa na Reiss (1971/2000). Nadharia hii inazingatia dhima ya lugha kama vile ujumbe au maudhui yanayohusiana na maarifa au sifa mahsusi za lugha ya matini katika kuainisha

matini kama vile matini za kisayansi na kisheria. Hivyo, tafsiri inapokuwa inafanyika izingatie aina ya matini husika. Anatoa kazi tano inazofanya nadharia hii katika tafsiri. Moja, ni kubainisha na kufasili tatizo la kifasiri yaani kazi au mlolongo wa shughuli za tafsiri zinazopaswa kufanywa katika utatuzi wa tatizo la tafsiri lililobainishwa. Pili, kuonesha vipengele vyote vinavyopaswa kuzingatiwa katika utatuzi wa tatizo la tafsiri lililobainishwa. Tatu, kuorodhesha taratibu au njia zote zinazowezekana kufanikisha tafsiri inayohusika. Nne, kupendekeza taratibu zinazofaa zaidi katika kutekeleza zoezi la kufasiri na tano, ni mbinu za kutafsiri zilizomuafaka zaidi kwa matini inayohusika.

2.4.2 Jinsi Nadharia za Ulinganifu Zilivyotumika katika Utafiti Huu

Katika utafiti huu nadharia za ulinganifu zilizotumika ni mbili. Tumetumia nadharia ya ulinganifu wa kidhima na ile ya ulinganifu wa aina za matini. Kwenye ulinganifu wa kidhima tuliangalia kama maudhui na ujumbe havikupotoshwa kutoka katika matini chanzi kwenda matini lengwa kwa kuangalia uzito na mguso sawa wa matini hizo. Kuhusu nadharia ya ulinganifu wa aina za matini, hapa tuliangalia umbo la ushairi kama limezingatiwa katika kufanywa kwa tafsiri kwa maana ya umbo la shairi chanzi na shairi lengwa. Nadharia hizi zilitumika katika kuyafikia malengo ya utafiti, ukusanyaji wa data, uchambuzi na uchanganuzi wake. Kwa kutumia misingi ya nadharia hii, mtafiti aliweza kulinganisha na kulinganua tafsiri hizi mbili na kujua sababu za mwachano wa tafsiri hizi pamoja na kujua changamoto za kutafsiri matini za ushairi na kisha kutoa matokeo ya utafiti.

2.5 Muhtasari wa Sura ya Pili

Sura hii imeongelea mapitio ya maandiko. Tumeangalia maandiko kuhusu maendeleo ya tafsiri ulimwenguni, maandiko kuhusu tafsiri katika fasihi na maandiko kuhusu tafsiri ya ushairi na changamoto zake. Aidha, maandiko kuhusu

Utenzi wa Omar Khayyam na tafsiri zake na maandiko kuhusu kulinganisha na kulinganua matini za kifasihi yameangaliwa. Baada ya kupitia maandiko hayo mtafiti alionesha mapengo ambayo yalihatiji kuzibwa na utafiti huu na kueleza nadharia alizozitumia katika utafiti wake.

SURA YA TATU

METHODOLOJIA YA UTAFITI

3.1 Utangulizi

Katika sura hii vipengele mbalimbali vimeshughulikiwa. Vipengele vilivyoshughulikiwa ni usanifu wa utafiti, eneo la utafiti, walengwa wa utafiti, jamii ya watafitiwa na usampulishaji na sampuli iliyotumika. Aidha, vipengele vingine ni ukusanyaji wa data, njia na zana za kukusanyia data, mchakato wa ukusanyaji wa data na uchanganuzi wa data. Pia, vipengele vya uzingatiaji wa itikeli ya utafiti, uhalali na uthabiti wa matokeo ya utafiti na mipaka ya utafiti vimetolewa ufafanuzi.

3.2 Usanifu wa Utafiti

Utafiti huu ulifanyika maktabani na uwandani. Kwa kuwa ulikuwa na mwelekeo wa kitaamuli haukijihusisha kabisa na data za kinumerari. Mkabala huu wa kitaamuli hutumia mbinu ya usanifu wa maelezo (ufafanuzi) unaoangalia thamani ya matini husika. Mbinu hii ya usanifu wa maelezo, inajikita katika kufafanua jambo bila kuhusisha taarifa za kitakwimu. Kwa hiyo, ukusanyaji, uchambuzi na uchanganuzi wa data pamoja na utoaji matokeo ya utafiti huu vimefanywa kwa kutumia mwelekeo huo wa kitaamuli. Sehemu kubwa ya data za utafiti huu zilipatikana maktabani kwa kuzikusanya kutoka katika maandiko mbalimbali yahasuyo tafsiri kwa ujumla. Vilevile, mtafiti alipata data kwa kuzamia zaidi tafsiri mbili za *Utenzi wa Omar Khayyam* ile ya Kiingereza ya Edward FitzGerald na ile ya Kiswahili ya Shaaban Robert. Data nyingine zilipatikana uwandani kwa njia za mahojiano na mijadala ya vikundi lengwa.

3.3 Eneo la Utafiti

Mahali pa utafiti huu, palikuwa Dodoma, Dar es Salaam, Zanziba na Mbeya. Sababu za uchaguzi huu ni upatikanaji wa wataalamu wa tafsiri na huduma ya maktaba

katika Chuo Kikuu cha Dodoma na Chuo Kikuu cha Dar-es Salaam ambapo mtafiti alipata maandiko mbalimbali ikiwemo tasnifu kuhusiana na mada yake. Pia, mtafiti alitalii mtandaoni ili kupata maandiko mbalimbali kuhusiana na mada yake.

3.4 Walengwa wa Utafiti

Walengwa wa utafiti huu waligawanywa katika makundi makuu mawili ambayo ni jamii ya watafitiwa na sampuli ya watafitiwa.

3.4.1 Jamii ya Watafitiwa

Ponera (2010) anaeleza dhana ya jamii ya watafitiwa kuwa, ni jumla ya vitu vyote ambavyo mtafiti anaweza kuvitumia kwa ajili ya kupata data za utafiti wake. Vitu hivi huweza kuwa kundi la watu, aina fulani ya wanyama, mimea au aina fulani ya maandiko. Hivyo, jamii ya watafitiwa iliyotumika katika utafiti huu ni:

- a) Wataalamu wa tafsiri toka Chuo Kikuu cha Dodoma na Chuo Kikuu cha Dar-es salaam;
- b) Wanafunzi wanaosoma kozi ya umahiri katika fasihi ya Kiswahili toka Chuo Kikuu cha Dodoma;
- c) Wanafunzi wanaosoma kozi ya tafsiri Shahada ya Kwanza Chuo Kikuu cha Dodoma; na
- d) Tafsiri mbili za *Utenzi wa Omar Khayyam* ile ya Kiswahili ya Shaaban Robert na ile ya Kiingereza ya Edward FitzGerald.

3.4.2 Usampulishaji na Sampuli Iliyotumika

Usampulishaji ni mchakato wa kupata sampuli inayohitajika na mtafiti. Kuhusu sampuli, Mligo (2012) anasema kuwa, ni kundi fulani la watu lililomo ndani ya mkusanyiko wa watu, ambalo mtafiti anaamini kwamba linazo habari zitakazomwezesha kujibu swali lake la utafiti. Hivyo, sampuli ya utafiti huu

ilipatikana kwa kutumia mbinu ya usampulishaji iso-bahatishi. Mbinu hii hutumika kupata sampuli iliyokusudiwa tu (kundi lengwa) na mtafiti. Mtafiti alitumia mbinu hii kwa sababu alihitaji kupata sampuli ya watu wenye uelewa wa kutosha juu ya mada yake pamoja na uelewa wa tenzi teule. Hivyo, sampuli ya utafiti huu iliundwa na makundi yafuatayo:

- a) Wahadhiri 4, wawili kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma na wawili kutoka Chuo Kikuu cha Dar-es - Salaam. Mtafiti ameweka idadi hiyo kulingana na upatikanaji wa wataalamu hawa katika uga wa tafsiri;
- b) Wanachuo 6 wa shahada ya umahiri katika fasihi ya Kiswahili toka Chuo Kikuu cha Dodoma. Mtafiti ameweka idadi hiyo ili kuweza kupata mawanda mapana ya mawazo toka kwa wanafunzi hawa; na
- c) Wanachuo 10 wa shahada ya kwanza wanaosoma kozi ya tafsiri katika Chuo Kikuu cha Dodoma kwa kuzingatia jinsia nusu kwa nusu. Mtafiti ameamua kutumia idadi hii ili kuweza kupata mawazo yenye mawanda mapana kuhusu tafsiri

3.5 Ukusanyaji wa Data

Sehemu hii inaeleza njia mbalimbali zilizotumika kukusanya data za uwandani na zile za maktabani, pamoja na zana zilizotumika kukusanyia data hizo.

3.6 Njia na Zana za Kukusanyia Data

Sehemu hii inafafanua njia na zana za kukusanyia data. Mtafiti alitumia mahojiano, mjadala na udurusu wa maandiko ili kukusanya data za utafiti wake.

3.6.1 Mahojiano

Mligo (2012) anasema kuwa mahojiano huweza kufanyika kati ya mtafiti na mtu mmoja mmoja au kati ya mtafiti na kundi la watu. Hii ni mbinu bora kutumiwa hasa

kwa utafiti wa kitaamuli kwani huhitaji ufafanuzi wa maelezo. Mbinu hii ilitumiwa na mtafiti kupata data toka kwa wahadhiri 4 na wanafunzi 6 wa Shahada ya Pili ya Fasihi ya Kiswahili Chuo Kikuu cha Dodoma. Mtafiti kwa kutumia daftari, kalamu na kinasa sauti alinukuu maelezo ya watafitiwa wake na kurekodi mazungumzo hayo yaliyomsaidia katika uchanganuzi wa data.

3.6.2 Majadiliano ya Vikundi

Majadiliano ni njia mojawapo aliyoitumia mtafiti katika kukusanya data ambapo watafitiwa hupangwa katika vikundi kadhaa kulingana na idadi inayofaa kisha kujadili mada iliyombele yao. Njia hii, alitumia mtafiti kukusanya data kuhusiana na changamoto za kutafsiri ushairi na matini nyingine za kifasihi na namna ya kuzitatua, sababu za mwachano wa tafsiri za *Utenzi wa Omar Khayyam* na kujadili mbinu mbalimbali zilizotumiwa na watafsiri wa *Utenzi wa Omar Khayyam* katika kufanya tafsiri. Njia hii ilitumika kwa wanachuo wa Shahada ya Kwanza katika Fasihi ya Kiswahili kujadili maswali kwa kufuata mwongozo wa majadiliano. Zana zilizotumika wakati wa ukusanyaji data ni kalamu na daftari kwa ajili ya kuandikia taarifa zinazotolewa. Pia, simu ilitumika kwa ajili ya kurekodi na kupiga picha.

3.6.3 Udurusu wa Maandiko

Udurusu wa maandiko ulitumika kukusanya data za utafiti maktabani. Maandiko yalimpatia mtafiti taarifa mbalimbali kuhusiana na mada yake. Udurusu wa maandiko ulimsaidia mtafiti, kupata ithibati juu ya utafiti wake kati ya data alizozipata uwandani na zile zilizopatikana maktabani kuzilinganisha kuona kama zinafanana au zinatofautiana. Mtafiti alitumia kalamu, karatasi na simu kwa madhumuni ya kunukuu taarifa muhimu anazozipata kutokana na udurusu wa maandiko na kuperuzi katika intaneti.

3.7 Mchakato wa Ukusanyaji wa Data na Udhibiti wake

Kabla ya mchakato wa kukusanya data kuanza, mtafiti ilimbidi kupata ruhusa ya kukusanya data kutoka uongozi wa chuo na kibali kilichomtambulisha katika maeneo aliyofanyia utafiti. Pia, ilimbidi kuandaa vifaa vinavyohitajika katika ukusanyaji wa data zake kwa kuzihakiki kama zinafanya kazi sawasawa. Alipokuwa uwandani ilimbidi kujitambulisha na kuomba ridhaa ya watafitiwa wake kama wako tayari kumpa taarifa anazozihitaji.

Data za uwandani zilikusanywa kwa kutumia njia ya mahojiano na mjadala. Mtafiti alifanya usaili kwa wahadhiri na wanachuo wa Shahada ya umahiri katika Fasihi ya Kiswahili. Aidha, alifanya mjadalakwa wanachuo wa Shahada ya Kwanza wanaosoma kozi ya tafsiri. Usaili huo ulinukuliwa na kurekodiwa kwa madhumuni ya kusaidia katika uchambuzi na uchanganuzi wa data. Data za maktabani zilikusanywa kwa kufuata mwongozo wa usomaji ulioandaliwa, amabo ulimwongoza mtafiti wakati wa kudurusu maandiko ili kupata data za utafiti.

3.8 Uchanganuzi wa Data

Mbinu iliyotumika katika uchanganuzi wa data za utafiti huu ni mbinu ya ufafanuzi. Sababu ya kutumia mbinu hii, ni kuwa sehemu kubwa ya data za utafiti huu zilizotarajiwa kukusanywa zilikuwa ni za maelezo. Maelezo hayo yalitokana na mahojiano na mjadala, pamoja na data za maktabani zilizokusanywa kulingana na malengo ya utafiti yaliyowekwa. Vielelezo vya picha pia vimetumika kuwasilisha baadhi ya matokeo na kutoa uthibitisho ambao kwa namna nyingine unahitaji kuthibitishwa kwa picha.

3.9 Uzingativu wa Itikeli ya Utafiti

Kwa mujibu wa Mligo (2012), itikeli ni uwajibikaji wa uelekevu kitabia kuhusiana na haki za wale wote tunaotangamana nao katika utafiti. Uelekevu huo upo katika nia na malengo ya utafiti na jinsi ya kuyatumia matokeo kwa uadilifu ili yaweze kuwa na faida kwa jamii ya binadamu. Naye, Chuachua (2016) anasema itikeli hushughulikia usahihi wa matendo katika mahusiano ya watu. Matendo hayo ni yale ambayo jamii imeyakubali kuwa ndiyo ya kuyatenda au kutoyatenda. Itikeli yaweza kuwa kwa kiwango cha kitaifa, kijamii, kikundi au umoja fulani, dini na hata weledi fulani kama vile ualimu, udaktari na kadharika. Kwa maana hiyo basi, utafiti uliozaa tasnifu hii ulifanywa kwa kuzingatia kanuni za kisayansi katika hatua zote za mchakato wa utafiti kama vile ukusanyaji wa data, uchambuzi wake, uchanganuzi wake na utoaji wa matokeo. Miongoni mwa kanuni hizo ni ile ya kuzingatia itikeli maalumu za kitafiti ili kulinda hadhi na utu wa wahusika wote wa utafiti. Pamoja na nyingine nyingi itikeli hizi hujumuisha masuala ya kuwa na ruhusa maalumu ya kufanya utafiti kutoka katika asasi au taasisi husika na uombaji wa ridhaa ya watafitiwa ili watafitiwe. Aidha, niwajibu wa mtafiti kuwafahamisha watafitiwa malengo ya utafiti na mambo mengine kuhusu utafiti huo pia kutunza siri na taarifa zitolewazo na watafitiwa na uzingativu wa maadili ya jamii za wahusika. Kwa hiyo, katika uendeshaji wa mchakato wa utafiti huu, masuala haya yalizingatiwa ipasavyo na mtafiti.

3.10 Uhalali na Uthabiti wa Matokeo ya Utafiti

Uhalali wa matokeo ya utafiti maana yake ni ile hali ya utafiti kutokuwa na kutiliwa mashaka ya aina yoyote ile, kutokana na mpangilio na taratibu kuhusu utafiti kama zilifuatwa inavyotakiwa. Uthabiti wa utafiti ni ile hali ya utafiti kutoa matokeo ambayo hata tafiti zingine zikifanyika kuhusiana na utafiti huo, matokeo hayatakuwa

mbali na yaliyopatikana katika utafiti huu. Hivyo basi, ili kupata matokeo thabiti na halali mtafiti alizingatia mada, malengo, maswali na mipaka ya utafiti. Aidha mtafiti alitumia nadharia ilinganayo na maudhui, walengwa wa utafiti, mbinu na zana sahihi za kukusanyia data. Pia, ukusanyaji, uchambuzi na uchanganuzi wa data ulizingatia itikeli na nadharia sahihi ya utafiti aliyoitumia mtafiti hatimaye kutoa matokeo ya utafiti

3.11 Mipaka ya Utafiti

Utafiti huu ulihusu tafsiri mbili za *Utenzi wa Omar Khayyam*, tafsiri ya Kiingereza ya Edward FitzGerald na ile ya Kiswahili ya Shaaban Robert katika kulinganisha na kulinganua tafsiri hizi mbili kuona wapi zinashikana na wapi zinaachana. Pamoja na hayo, utafiti huu uliangalia changamoto zinazojitokeza katika kutafsiri ushairi na namna ambavyo zinaweza kutatuliwa.

Utafiti ulipitia maandiko na tasnifu mbalimbali ili kupata ufahamu wa kutosha juu ya tafsiri ya ushairi kwa kuangalia tafsiri mbili za *Utenzi wa Omar Khayyam* ile ya Kiingereza ya Edward FitzGerald na ile ya Kiswahili ya Shaaban Robert. Mtafiti aliangalia jinsi zinavyolingana na jinsi zinavyotofautiana na sababu za mwachano huo.

3.12 Changamoto Zilizojitokeza na Utatuzi Wake

Utafiti huu ulikumbana na changamoto kadhaa. Kwa kuwa utafiti huu kwa data za uwandani kwa kiasi kikubwa ulikuwa ni wa kuwahoji wataalamu wa tafsiri, changamoto za kubadilika kwa ratiba ya kukutana na wataalamu hawa zilijitokeza. Kwa mfano, mtafiti ameahidiwa kuonana na mtaalamu siku ya Jumatatu, lakini inapofika siku hiyo anapewa ratiba ya siku nyingine. Changamoto hii ilitatuliwa kwa kukubaliana na ratiba mpya.

Changamoto nyingine iliyojitokeza kwa wataalamu hawa, badala ya kujibu maswali ya mtafiti yeye ndiye anakuwa muuliza maswali na mtafiti kujibu maswali ambayo mara nyingine hayahusiani na maswali ya utafiti. Changamoto hii ilitatuliwa kwa mtafiti kumrudisha mtafitiwa kwenye mstari kisha mahojiano kuendelea kufanyika.

Changamoto ya mwisho iliyojitokeza ni kwa watafitiwa kutokuwa na uelewa wa kutosha juu ya kazi za Omar Khayyam. Kazi hizi zilionekana ngeni kwa watafitiwa hasa watafitiwa wa Shahada ya Umahiri na wale wa Shahada ya Kwanza. Changamoto hii ilitatuliwa kwa mtafiti kulazimika kutoa ufafanuzi kidogo juu ya kazi za mshairi Omar Khayyam hasa utenzi huu.

3.13 Muhtasari wa Sura ya Tatu

Sura hii imeongelea methodolojia ya utafiti kwa kugusia usanifu wa utafiti, eneo la utafiti, walengwa wa utafiti, jamii ya watafitiwa na sampuli na usampulishaji. Aidha, kumeongelewa ukusanyaji wa data, njia zilizotumika katika kukusanya data, mchakato wa ukusanyaji data, uchanganuzi wake pamoja na kuonesha mipaka ya utafiti na changamoto za utafiti na jinsi zilivyotatuliwa.

SURA YA NNE

UWASILISHAJI NA MJADALA WA MATOKEO YA UTAFITI

4.1 Utangulizi

Sura hii inawasilisha na kujadili matokeo ya utafiti. Sura ina sehemu sita ambazo ni utangulizi, maelezo mafupi juu ya jamii ya Waajemi, mbinu zilizotumika kutafsiri *Utenzi wa Omar Khayyam*. Aidha kumejadiliwa kufanana na kutofautiana kwa tafsiri za *Utenzi wa Omar Khayyam*, sababu za kuwapo kwa mwachano wa tafsiri hizi na muhtasari wa sura hii. Mjadala umefanywa ili kuthibitisha pamoja na kuonesha ulinganifu na ulinganuzi wa tafsiri mbili za *Utenzi wa Omar Khayyam* ile ya Kiingereza ya Edward FitzGerald na ile ya Kiswahili ya Shaaban Robert. Mjadala huuumeongozwa na nadharia za ulinganifu, hususani nadharia ya ulinganifu wa kimaudhui na ile nadharia ya ulinganifu wa umbo la matini.

4.2 Jamii ya Waajemi

Kwa mujibu wa *Wikipedia the free encyclopedia* (2016), Waajemi ni miongoni mwa jamii za Kiirani ambapo jamii hii inafanya nusu ya Wairani wote. Richard (1998) anasema kuwa, Waajemi wana utamaduni wao wa pamoja kuhusiana na lugha yao ya Kiajemi ambayo huzungumzwa miongoni mwao. Kuhusiana na utamaduni wao na namna wanavyoathamini utamaduni huo wanajitahidi kuulinda pamoja na kuwa kwa sasa una mwingiliano mkubwa. Mwandishi kusema:

Persian now had a choice, they could accept a new culture including nationality language (Arabic and religion Islam) or they could hold tight to the unique attributes making up their Persian identities. Any one who has heard of Persian pride knows they fought to remain as Persian not Arabs (pg xxii).

Waajemi kwa sasa wanalazimika kupokea utamaduni mpya ikiwemo lugha ya taifa (Kiarabu na dini ya Kiislamu) au washikilie mila na desturi zao zinazowatofautisha na kuwafanya waonekane kama

Wajemi. Yeyote anayesikia ufahari wa Kiajemi ni ile hali ya kubaki Mjemi na si Mwarabu (tafsiri ya mtafiti).

Maelezo hayo yanatuonesha namna ambavyo utamaduni na uatambulisho wa Wajemi unavyokabiliwa na msukumo wa kitaifa kwa upande mmoja na jinsi Wajemi wanavyojitahidi kushikilia utamaduni wao usipotee. Kuhusiana na mambo ya ushairi Wajemi wanasifika sana katika utunzi wa ushairi na katika maandiko ya kifasihi. Kuna kazi nyingi sana za ushairi kwa lugha ya Kiajemi. Lois (2014) kuhusiana na ushairi wa Wajemi anaeleza kuwa ni maarufu na ni ushairi mzuri. Mwandiahi anasema:

Persian language become the major literary instrument for many poems and religious works. Persian poetry is some of the most beautiful poetry in the world and the Persian cultivated from unique types of poetry (pg 40).

Lugha ya Kiajemi imekuwa zana muhimu ya uandishi katika ushairi na kazi za kidini. Ushairi wa Kiajemi ni miongoni mwa ushairi mzuri ulimwenguni na Wajemi walianzisha aina yao pekee ya ushairi (tafsiri ya mtafiti).

Maelezo hayo yanatuonesha kuwa ushairi na lugha ya Kiajemi ni vitu vinavyoenda sambamba hadi kufikia kusifiwa kuwa mashairi ya Kiajemi ni miongoni mwa mashairi mazuri sana. Kuhusiana na mambo ya dini, Wajemi kabla ya Uislamu walikuwa na dini yao inayoitwa *zoroastrianis*. Maelezo haya yanashadidiwa na Richard (1998) anasema:

Prior to the foundation of Islam in Iran, Persian are noted for the development of one of the oldest monotheistic religion Zoroastrianism. In this religion there is one Lord wisdom known as Ahura Mazda. Also important to the religion is the concept of the nature of good (Senta mainyu) and evil (Angra mainyu). One can see how the later monotheistic religion of Judaism, Christianity and Islam have taken many of their teachings from this religion Zoroastrianism, while having a small following, is still practice today and many Iranian festivals still center around the Zoroastrian calendar. One favorite is Norooz, a celebration of the Iranian new year taking place on the spring Equinox (pg 80-83).

Kabla ya misingi ya Kiislamu katika nchi ya Iran, Waajemi walitambulika kuwa na dini yao iitwayo Uzorostiani. Katika dini hii kuna Mungu wa hekima mmoja anayejulikana kama Ahura Mazda. Kitu kingine cha muhimu katika dini hii ni dhana ya asili ya mema (Senta mainyu) na ubaya (Angra mainyu). Tunaweza kuona athari za dini hii katika dini ya Kiyahudi, Kikristo na Kiislamu ambazo zimechukua mafundisho mengi kutoka katika dini ya Uzoroastriani, pamoja na kuwa na wafuasi wachache bado inaabudiwa mpaka sasa na matamasha mengi ya Kiirani yamejikita katika kalenda ya *zoroastrian*. Moja ya tamasha linalopendwa zaidi ni Norooz, ni sherehe ya Wairani ya mwaka mpya ambayo hufanyika majira ya masika (tafsiri ya mtafiti).

Maelezo hayo yanatuonesha mila na desturi za Waajemi katika dini na namna ambayo inasemekana dini yao ilianza zamani kabla ya dini hizi tunazoziona na kabla ya Uislamu na Ukristo, kwa hiyo dini kwao ni sehemu ya utamaduni wao tangu zamani.

4.3 Mbinu Zilizotumika Kutafsiri *Utenzi wa Omar Khayyam*

Lengo mahsusi letu la kwanza lilikuwa ni kuchunguza mbinu zilizotumiwa na Edward FitzGerald na Shaaban Robert kutafsiri *Utenzi wa Omar Khayyam*. Ngugi (2010) anazungumzia mbinu za kutafsiri matini za kifasihi kuwa ni kuzingatia umbo la matini kwa maana ya aina ya matini husika. Naye, Mungai (2005) anasema kuwa tafsiri yoyote ile huhitaji kutilia maanani elementi za kimazingira kuhusu wasomaji kabla ya kuamua ni mchakato gani utakaofuatwa katika kutafsiri. Mwansoko (2013) anasema kuwa katika kufasiri ushairi ni muhimu kila neno katika mstari na kila mstari katika ubeti vishughulikiwe na kuzingatiwa kwa uzito uleule. Hapa, tunaona wataalamu hawa wakigusia baadhi ya mbinu zinazotumika katika kutafsiri matini za kifasihi. Kabla ya kuanza kuziangalia mbinu hizo, tuangalie kwanza maelezo kwa ufupi kuhusiana na tafsiri hizi.

4.3.1 Muhtasari wa Tafsiri za Utenzi wa Omar Khayyam

Kama ilivyoielezwa huko mwanzo kuwa, utenzi huu umefanyiwa tafsiri nyingi sana. Kwa muktadha wa kazi yetu, tutaangalia muhtasari wa tafsiri ya Kiingereza ya Edward FitzGerald na ile tafsiri ya Kiswahili ya Shaaban Robert.

4.3.1.1 Muhtasari wa Tafsiri ya Edward FitzGerald

Kwa mujibu wa *Wikipedia the free encyclopedia* (2017), Uingereza ni moja ya nchi zilizo katika muungano wa nchi za Ufalme wa Kiingereza (*United Kingdom*). Watu wake wengi wanaongea lugha ya Kiingereza ambayo ni lugha maarufu ulimwenguni. Lugha hii imeenea ulimwenguni kote kutokana na taifa la Uingereza kuwa na makoloni ulimwenguni kote ambako kila walikotawala walieneza lugha yao ya Kiingereza na kufanya maandiko mengi duniani kuwa ya Kiingereza. Kumar (2013) anashadidia hili akieleza sababu ya kuenea lugha hii ulimwenguni anasema kuwa, *due to the expansion of English into a world language during The British Empire, literature is now written in English across the world* (kwa sababu ya kupanuliwa kwa lugha ya Kiingereza katika ulimwengu wakati wa himaya ya Waingereza fasihi inaandikwa kwa lugha ya Kiingereza ulimwenguni kote) kwa hiyo tunapoongelea jamii ya Waingereza kwa maana ya wazungumzaji wa lugha, tunaongelea ulimwengu mzima.

Kuhusu dini Waingereza wengi ni waumini wa Ukristo kiasi cha kuifanya dini hiyo kuwa ni dini ya taifa la Uingereza. Dini hii ililetwa na Warumi mnamo karne ya saba kama ambavyo Kumar (khj) anasema kuwa, *Christianity become the dominant religion in England in the 7th century. Christianity was first established in Britain by the Roman Empire* (Ukristo ulikuja kuwa dini kuu katika Uingereza karne ya saba. Ukristo ulianzishwa Uingereza na dola la Warumi) Kwa hiyo tunapokuwa tunazungumzia mambo ya dini kwa Mwingereza Ukristo ndiyo dini yake.

Utenzi wa Omar Khayyam ulitafsiriwa kwa mara ya kwanza na Edward FitzGerald kwa lugha ya Kiingereza mnamo mwaka 1859 kutoka lugha ya Kiajemi. Tafsiri hiyo ya lugha ya Kiingereza ya Edward FitzGerald ina chapa ya kwanza hadi ya tano. Kwa muktadha wa utafiti wetu, tunashughulika na tafsiri chapa ya kwanza, ambayo ina jumla ya beti 90. Maudhui makuu ya tafsiri hii yanahusu dini, hasa dini ya Kiislamu. Kwa mfano, ubeti wa 73 unadhihirisha maudhi ya dini ya Kiislamu ambapo kunatajwa maneno kama vile Ramazan na Mfungo mosi. Mambo mengine yaliyojadiliwa katika tafsiri hii ni mambo kuhusu maisha ubeti wa 7 na 9 Pia, mambo yanayohusiana na madaraka au uongozi yanapatika katika ubeti wa 13,15, 16, na 17 Aidha, mambo yanayohusiana na mapenzi yamedhihirika katika ubeti wa 22, 23, na 24. Utenzi huu pia unaongelea masuala ya uumbaji wa Mungu na historia ya mwanadamu alivyoumbwa. Mambo haya yandhihirika katika ubeti wa 74 hadi 81. Pia, tafsiri hii ina muundo wa beti zenye mishororo minne ikizingatia mtindo wa urari wa vina na mizani.

4.3.1.2 Muhtasari wa Tafsiri ya Shaaban Robert

Kipacha (2003) akizungumzia lahaja za Kiswahili anasema kuwa, jamii ya Waswahili kwa kuzingatia jiografia ni watu wa mwambao wa pwani ya Afrika Mashariki ambao ndani yake tunakutana na lahaja mbalimbali za Kiswahili (Kikitukuu, Kikipate, Kimvita, Kingozi na Kingwana) na tunapokuwa tunazungumzia jamii ya Waswahili kwa maana ya wazungumzaji, tunamaanisha watu wote wenye uwezo wa kuzungumza Kiswahili popote walipo ulimwenguni.

Utenzi wa Omar Khayyam ulitafsiriwa kwa lugha ya Kiswahili na Shaaban Robert mnamo mwaka 1948 kutoka tafsiri ya Kiingereza ya Edward FitzGerald chapa ya kwanza. Utenzi huu wa Kiingereza uliletwa kwa Shaaban Robert na A. A. M. Isherwood wa iliyokuwa idara ya elimu *Tanganyika Territory* pamoja na barua ya

kumtaka Shaaban Robert atafsiri utenzi huo kwa Kiswahili. Robert (1973) anaeleza kuwa aliletewa tafsiri hii mwaka 1944 naye baada ya kumaliza kuifanya kazi hiyo mwaka 1948 aliandika barua kumjulisha Bw, Isherwood kuhusu kukamilika kwa kazi hiyo; mwandishi anasema:

Kitabu cha mashairi ya Kiingereza ilimotoka tafsiri hii kililetwa kwangu na Bwana A. A. M. Isherwood, C. M. G. Mudir wa Idara ya Elimu, *Tanganyika Territory* pamoja na barua ya kunitaka nifanye tafsiri (uk 103-104).

Utenzi huu kwa tafsiri ya Kiswahili una beti 67 ambazo zinazungumzia masuala ya dini ya Kiislamu. Mambo mengine ni kuhusu maisha ubeti wa 7 na 8, madaraka na uongozi ubeti wa 12,13, 14, na 15. Pia, kumezungumzwa mambo kuhusu mapenzi ubeti wa 20, 21, na 22. Mbali na hayo, mambo mengine yaliyozungumzwa ni kuhusu kifo ubeti wa 21, 23 na 49 pamoja na historia ya kuumbwa kwa binadamu katika ubeti wa 60 hadi 67.

Kama ilivyoelezwa hapo juu kuwa, matini chanzi ina beti 90, ilhali tafsiri hii ya Kiswahili ina beti 67. Tofauti hii imesababishwa na baadhi ya beti kutotafsiriwa kabisa kutoka katika matini chanzi. Kwa mfano, Shaaban Robert hakutafsiri kabisa jumla ya beti 26 na alitunga beti mpya tatu ambazo ni ubeti wa 30, 41 na 44. Pia, utafiti umebaini kuwa mpangilio wa tafsiri hii unaenda sawa kwa namba za beti kuanzia ubeti wa kwanza hadi wa saba, baada ya hapo kuna mpishano mkubwa. Mpishano wa beti katika tafsiri hii unamtaka msomaji awe makini katika kuoanisha beti hizo zilizotafsiriwa kwani haziendani kinamba.

Kwa mujibu wa McCathy (1889), tafsiri ya Kiingereza ya *Utenzi wa Omar Khayyam* iliyofanywa na Edward FitzGerald ni tafsiri ya kwanza ya Kiingereza kutoka kwenye matini chanzi ya Kiajemi. Tafsiri ya Kiswahili ya Shaaban Robert ni tafsiri iliyotokana na tafsiri; kwa maana hiyo, tafsiri ya Shaaban Robert ni tafsiri ya tafsiri.

4.3.2 Mbinu Walizotumia Edward FitzGerald na Shaaban Robert Kutafsiri

Utenzi wa Omar Khayyam

Utafiti huu umegundua kuwa, watafsiri Edward FitzGerald na Shaaban Robert katika kutafsiri *Utenzi wa Omar Khayyam* walitumia mbinu zifuatazo:

4.3.2.1 Uzingatizi wa Umbo la Matini Chanzi

Mulokozi na Kahigi (1979), wakiongelea umbo la matini za kishairi, wanasema kuwa, ni ule mpangilio maalumu wa maneno fasaha na yenye muwala kwa lugha ya mkato, picha au sitiari au ishara, katika usemi, maandishi, au mahadhi ya wimbo ili kuelezea wazo au mawazo, kufunza au kueleza hisi fulani, kuhusu maisha au mazingira ya binadamu kwa njia inayogusa moyo.

Wataalamu wengi wametaja mbinu mbalimbali za kutafsiri ushairi, ikiwemo kutafsiri shairi kwa kuzingatia maudhui. Ili kulinda maudhui mama ya matini chanzi, ni muhimu kulitunga shairi upya, kutafsiri shairi kwa kuzingatia tamaduni za lugha lengwa, kutafsiri shairi kwa kuzingatia mazingira na kutafsiri shairi kwa kuzingatia umbo la matini chanzi. Mwansoko (2013) anasema kuwa tafsiri nzuri ni ile yenye kusema vilevile kama yasemavyo makala yaliyotafsiriwa na iwe inalingana na maandishi asili. Mambo mengine anayoyataja ni pamoja na matini hiyo ieleze mambo kama kwamba lugha iliyotumiwa ndiyo lugha asili iliyotumiwa kuandika makala hayo; na mwisho, izingatie umbo la matini chanzi.

Kwa kuzingatia nguzo kuu za nadharia za ulinganifu katika utafiti huu, ulinganifu wa kidhima na ulinganifu wa aina ya matini au umbo la matini. Mshairi Omar Khayyam anelezwa na wataalamu kama vile Yogananda (1920) kuwa, alikuwa mtunzi wa mashairi ya *rubaiyat* (unne) na kuzingatia urari wa vina na mizani na yanazungumzia zaidi masuala ya kidini. Hivyo, Edward FitzGerald alipokuja

kutafsiri utenzi huu alizingatia umbo la ushairi kwa kufuata mishororo minne na urari wa vina na mizani. Kwa hiyo, utenzi mzima aliutafsiri kwa kuzingatia umbo la ushairi. Beti zifuatazo katika lugha ya Kiajemi zilizopatikana kwa msaada wa mtandao zinathibitisha hili:

خوششید کند صبح بر بام آن کند
کنجشور و روز باوه در جام آن کند
می خور که منادی سحر که خیزان
آواز ز اشربو در ایام آن کند

1 AWAKE! For Morning in the Bowl of Night,
Has flug the stone that puts the stars to Flight,
And Lo! The Hunter of the East has Caught,
The Sultan's Turret in a Noose of Light.

چندان بخورم شراب کاین بوی شراب
آید ز تراب چون روم زیر تراب
مگر برسد قبر من رسد مخموری
از بوی شراب من شود مستی شراب

3. And, as the cock crew, those who stood before
The Tavern shouted- open the Door
You know how little while we have to stay
And once departed, may return no more

با تو بجز اباست اگر گویم راز
بزرگد بجز اب کهنم راز و نیاز
ای اول و ای آخر خلتان همه تو
خواهی تو مرا بسوز و خواهی سوز

67 And this I know: Whether the one True Light
Kindle to Love, or Wrath Consume me quite
One Glimpse of It within the Tavern caught
Better than in The Temple outright

بر کوزه گری پریر کردم گدزی
از خاک بی نمودم بروم هنری
من دیدم اگر ندیدم بر بی بصری
خاک پدرم و کف بر کوزه گری

73. Listen again, One Evening at the Close
Of Ramazan ere the better Moon arose
In that old Potter's Shop I stood alone
With the clay Population round in Rows

Beti hizo zinazungumzia maisha ya kawaida ya binadamu; kwamba, panapokucha wanatakiwa waamke, maana jua limechomoza. Pia, mwandishi anaendelea kuelezeakuwa, jogoo amewika hivyo, watu wanatakiwa waamke wafanye kazi maana baada ya kifo hakutakuwa na kumbukumbu tena ya maisha yao. Kwa kuangalia mifano ya beti hizo nne hapo juu tunaona kuwa mtafsiri Edward FitzGerald alizingatia utunzi wa mashairi ya mishororo minne na yenye kufuata kanuni za vina na mizani kama mtunzi asili wa utenzi huu alivyofanya. Kwa upande wa Shaaban Robert alipotafsiri, hakuzingatia umbo la shairi husika kwa maana ya mishororo. Kwa mfano, badala ya mishororo minne, yeye aliweka mishororo minane

kwa kila ubeti. Haijulikani ni sababu zipi zilizomfanya aamue kufanya hivyo, pengine aliamua kufanya hivyo ili kukidhi haja ya kuhusisha muundo na jina husika yaani utenzi. Sifa mojawapo ya utenzi ni kuwa na beti nyingi zaidi kuliko shairi; na huwa unakuwa na mizani minane tu katika kila mshororo. Msokile (1991), akichambua na kuhakiki mashairi ya *Karibu Ndani*, anaeleza tofauti iliyopo kati ya shairi na tenzi. Anasema kuwa tenzi ni ndefu kuliko mashairi ya kawaida, zinaweza kuwa na beti hadi elfu nne au zaidi; na mara nyingi, huongelea wazo moja kwa mwendelezo wa ubeti mmoja na mwingine. Pamoja na hayo, tunaweza kusema kuwa Shaaban Robert alitafsiri kwa kuzingatia mtindo wa shairi chanzi, huku akifuata mtindo wa vina na mizani katika tafsiri yake. Beti zifuatazo zinathibitisha hili:

1. *L.L. AWAKE! For Morning in the Bowl of Night
Has flug the stone that puts the stars to Flight
And Lo! The Hunter of the East has Caught
The Sultan's Turret in a Noose of Light*

1. L.C. *AMKENI!* Asubuhi imerusha
Jiwe katika Giza
Ambalo limeondosha
Nyota na kuzifukuza
Tena kumbe! Limekwisha
Jua juu kutokeza
Nuru yake imewasha
Mnara unaangaza

3. L.C. *And, as the cock crew, those who stood before
The Tavern shouted- open then the Door!
You know little while we have to stay
And once departed, may return no more*

L.L. Jogoo lilipolia
Watu waliosimama
Mbele ya Mkahawa
“Fungua Mwango” waasema
Maisha mwaelewa
Kuwa mafupi daima
Haturudii dunia
Mara moja tukihama

7. L.C. *Come, fill the cup, and in the Fine of spring*
The winter Garment of Repentance fling
The Bird of Time has but a little way
To fly- and Lo! The Bird is on the wing

L.L. Njoo ujaze Kikombe
Huzuni yako ivue
Isikate kama wembe
Katika moto itie
Haya maisha ni chembe
Kama ndege mfanowe
Ghafula hii kumbe
Huruka kwa mabawaye

Tukiangalia beti hizo hapo juu, tunaona kuwa mtafsiri Shaaban Robert hakuzingatia umbo la shairi chanzi katika upande wa mishororo, bali alichangalia ni uzingativu wa vina na mizani. Kama ilivyoelezwa hapo juu, haijulikani kwa nini aliamua kutumia muundo huo. Yawezekana alifanya hivyo ili kukidhi haja ya sifa ya utenzi kuwa na mishororo zaidi ya minne na mizani minane katika kila mshororo. Aidha, utenzi huongelea jambo moja kwa mtindo wa ubeti mmoja ukifuatiwa na mwingine kama ambavyo utenzi huu kwa kiasi kikubwa unaongelea mambo ya dini.

4.3.2.2 Uzingatizi wa Maudhui

Mbinu nyingine waliyotumia Edward FitzGerald na Shaaban Robert ni kutafsiri kwa kuzingatia dhima au maudhui yaliyomo katika kila ubeti. Nadharia ya ulinganifu wa kidhima inaeleza kuwa inampasa mtafsiri atafsiri kwa kuzingatia maudhui yaliyopo katika matini chanzi. Maudhui hayo yasawiri muonjo na mguso wa matini chanzi na kusikika vilevile katika matini lengwa. Makaryk (1993) anasema kuwa tafsiri ya ulinganifu wa kidhima isionekane kuwa tafsiri, bali kazi asilia katika lugha lengwa. Kwa hiyo, mfasiri lazima atafute visawe linganifu katika lugha lengwa ambavyo ni vya karibu zaidi na ujumbe wa lugha chanzi. Mawazo hayo, kwa kiasi fulani, yanaungwa mkono na Mshindo (2010) anaposema kuwa, siyo rahisi kupata tafsiri timilifu isipokuwa kinachotakiwa ni kupata tafsiri toshelevu ambayo inakidhi

matakwa ya mfasiri na msomaji kwa maana ya ujumbe uliokusudiwa kufika kwa mlengwa.

Kwa hiyo, kama ilivyoelezwa awali mashairi mengi ya mtunzi Omar Khayyam yalikuwa na maudhui ya kidini hasa dini ya Kiislamu. Omar Khayyam ameongelea mambo ya uumbaji na mahusiano ya Mungu na mwanadamu, jinsi mwanadamu alivyoumbwa kwa udongo na anamfananisha Mungu kama Muumbaji na mwanadamu kama chombo kilichoumbwa kwa udongo. Maneno haya yanasawiri imani ya dini, kwani waumini wanaamini kuwa mwanadamu aliumbwa kwa udongo kisha akapuliziwa na Mungu pumzi ya uhai, mtu akawa nafsi hai (Mwanzo 2:7).Beti zifuatazo zinathibitisha hili:

*71. Oh Thou, who Man of baser Earth didst make
And who with Eden didst devise the Snake
For all the sin wherewith the Face of Man
Is blacken'd Man's Forgiveness give – and take!*

Ewe uliyemwandaa
Kwa Udongo Mwanadamu
Na ambaye ulizua
Nyoka Eden kudumu
Dhambi imeumbua
Uso wake Mwanadamu
Msamaha pokea
Atoapo Mwanadamu

*73 Listen again. One Evening at the Close
Of Ramazan, ere the better Moon arose
In that old Potter's Shop I stood alone
With the clay Population round in Rows*

Tena sikilizeni
Siku moja jioni
Mwisho wa Ramadhani
Mfungomosi jirani
Kwa Mfinyanzi dukani
Nilikuwa pweke ndani
Watu wa Udongo ndani
Walisimama Safuni

*74 And strange to tell, among that Earthen Lot
Some could articulate, while others not
And suddenly one more impatient cried –
Who is the Potter, pray, and who the Pot?*

Ni ajabu kwa hakika
Habari za watu hawa
Wengine walitamka
Wengine walinyamaa
Mmoja alitamka
Kwa kushindwa vumilia
Mfinyanzi ningetaka
Na Chombo kuelezewa

*75 Then said another – Surely not in vain
My Substance from the common Earth was ta'en
That He who subtly wrought me into shape
Should stamp me back to common Earth again*

Si kazi bure kweli
Wa pili jibu katoa
Mimi wangu mwili
Chini ulichimbuliwa
Katika umbo hili
Aliyenifanya kuwa
Kama vile awali
Chini tena nitatiwa

*76. Another said- Why, ne'er a peevis Boy
Would break the Bowl from which he drank in Joy
Shall He that made the vessel in pure Love
And Fancy, in an after Range destroy?*

Kwa nini Mtoto mtukutu
Mwingine alijibu
Atakivunjaje kitu
Kwa raha alichonywea Wahabu
Aliyekifanya kitu
Kwa mapenzi taratibu
Wadhaniaje tu
Atakivunja kwa Ghadhabu

Tukiangalia maudhui ya beti hizo tunagundua kuwa yanaongelea mambo yadini jinsi binadamu alivyoubwa na anavyotakiwa kuishi katika ulimwengu kwa kumtumaini Mungu. Msingi unaojengwa na dhana hii ni ufupi wa maisha ya mwanadamu hapa duniani. Mbali na hayo, mtafsiri Edward FitzGerald anaongeza kuwa binadamu

katika maisha yake hapa duniani afanye mambo yake kwa nguvu zote, kwani baada ya kufa hawezi kurudi tena kwani yeye ni mavumbi na mavumbini atarudi. Beti hizo zimetungwa kama masimulizi fulani hivi; hii ni kuonesha tu ubunifu wa Omar Khayyam katika kutunga mashairi. Kwa maana hiyo, Edward FitzGerald alizingatia maudhui ya matini chanzi ya Kiajemi kama tulivyodokeza kuwa mashairi ya Omar Khayyam maudhui yake makuu yalikuwa ni ya kidini.

Shaaban Robert katika kutafsiri utenzi huu nayealizingatia maudhui. Uzingatizi huu, hufanywa na mtafsiri kwa lengo la kufikisha ujumbe kwa kuzingatia maudhui yaliyokusudiwa kwa maana ya muonjo sawa kama vile matini chanzi ilivyo katika uzito, utamu na mguso. Abdulmalick¹ anataja mbinu mojawapo itumikayo kutafsiri kuwa ni kutafsiri kwa kuangalia maudhui ya matini chanzi. Anaona kuwa hapa kinachozingatiwa ni maudhui au matini husika ili ujumbe uweze kufika kwa walengwa kama ilivyokusudiwa. Mawazo haya yanaungwa mkono na Nathan (2006) alipokuwa akizungumzia tafsiri kwa watu wenye mahitaji maalumu anasema kuwa, maudhui ndio kitu cha msingi na cha kuzingatiwa katika tafsiri. Ili kuthibitisha hili tuangalie beti zifuatazo:

22. L.C. *Ah, my Beloved, fill the cup that clears
To-day of past Regrets and future Fears
To-morrow? Why, To-morrow I may be
My self with Yesterday's sev'n Thousand Years*

L.L. Aha, mpenzi wangu
Jaza bilauli hiyo
Initoe machungu
Ya zamani niwazayo
Tena iondoke kwangu
Hofu ya kesho ijayo
Kama sabiini kwangu
Jana nitakuwa nayo

¹ Mahojiano kati ya Mtafiti na Dkt. Feruz Abdulmalick wa Chuo Kikuu cha Dodoma yalifanyika tarehe 20/02/2018 Ofisi kwake. Huyu ni mtaalamu wa masuala ya fasihi na anasomesha katika chuo hiki.

16 .L.C. *The worldly Hope men set their Hearts upon
Turns Ashes- or it prospers and anon
Like snow upon the Deserts dusty Face
Lighting a little Hour or two- is gone*

L.L.Ulimwengu mpendao
Hugeuka majivu
Ghafula wabarikio
Hupatwa na ulegevu
Theluji mfano wao
Juu ya jangwa kavu
Saa moja ya mng'ao
Hapana tena uangavu

9. L.C. *Morning a thousand Roses brings, you say
Yes, but where leaves the Rose of Yesterday?
And this first summer Month that bring the Rose
Shall take Jamshyd and Kaikobad away*

L.L.Siku ikipambazuka
Elfu yanachanua
Elfu hutawanyika
Na kupotea maua
Msimu ukifika
Wa waridi kuchanua
Jamshyd atashika
Na Kaikobad njia

Tukichunguza tafsiri hiyo hapo juu tunagundua kuwa Shaaban Robert alikuwa anaamua kutafsiri maneno kwa kuweka visawe vyake vipya ili aweze kukidhi maana na maudhui ya ubeti husika. Dhima ya kufanya hivi ni kumfanya msomaji wake aweze kusikia mguso na utamu wa matini kama ulivyo katika matini chanzi. Hii ni mbinu inayoshauriwa na wataalamu wengi wa tafsiri itumike. Hii ni kwa sababu huifanya matini lengwa kuwa kama matini chanzi. Kwa mfano, kwenye ubeti wa kwanza mshororo wa tatu kuna maneno *'To – morrow? Why, To morrow I may be'* mshororo huu Shaaban Robert hakuutafsiri kabisa; badala yake, aliweka maneno *'hofu ya kesho ijayo'* ili kufikisha ujumbe. Katika ubeti wa pili kuna mshororo wenye maneno *'Lighting a little Hour or Two – is gon'*. Shaaban Robert ameutafsiri mshororo huo kwa maneno *'Saa moja ya mng'ao hapana tena uangavu'*. Pia, katika ubeti wa tatu kuna neno *'Morning'* Shaaban Robert ametafsiri kama *'Siku*

ikipambazuka'. Hali kadhalika, neno 'rose' ametafsiri 'maua'. Maneno mengine ni 'First summer' ambayo Shaaban Robert ameyatafsiri kama 'msimu ukifika' wakati kwa Waingereza 'summer' ni msimu maalumu unaojulikana na kila mtu na huenda ndio msimu ambao maua haya ya rose huchanua. Utafiti huu umegundua kuwa, mtafsiri aliamua kuyatafsiri maneno hayo kwa jinsi hiyo ili kulinda maudhui. Aidha, jamii anayoitafsiria iweze kula kazi yake kwa mguso sawa kama ilivyo katika matini chanzi, maana angetafsiri kama maneno yalivyo huenda jamii yake isingeweza kuupata ujumbe kama alivyokusudia.

4.3.2.3 Uzingatizi wa Utamaduni wa Jamii ya Lugha Lengwa

TUKI (1981) wanasema kuwa, utamaduni ni jinsi binadamu anavyoyakabili maisha katika mazingira yake. Hivyo, inajumuisha ujuzi, imani, sanaa, maadili, sheria na desturi ambavyo mtu anajipatia kama mwanajamii. Naye, Ponera (2014) anasema kuwa, utamaduni ni dhana ya jumla inayobeba dhana nyinginezo kama vile matumizi ya lugha, mitazamo ya kijamii, matumizi ya mavazi, misingi ya kimaadili ya jamii husika na sanaa za jadi.

Watafsiri Edward FitzGerald na Shaaban Robert walitumia mbinu ya kuzingatia utamaduni wa jamii ya lugha lengwa. Ikumbukwe kuwa, lugha ya awali ya utenzi huu ni Kiajemi na dini ya Omar Khayyamni Mwislamu. Kwa hiyo, wakati anatunga kazi yake alitunga kwa kuzingatia utamaduni wa watu wa Mashariki ya Kati kwa kujikita zaidi katika imani ya dini ya Kiislamu. Mkinga (2005) akielezea changamoto za kutafsiri dhana za kiutamaduni anasema kuwa, ni muhimu mtafsiri aufahamu vizuri utamaduni wa jamii zote mbili. Hivyo basi, mtafsiri anapaswa kuzingatia utamaduni wa lugha chanzi na ule wa lugha lengwa. Edward FitzGerald alitafsiri kwa kuzingatia tamaduni za Waingereza na wenye imani ya Kikristo ili hadhira yake iweze kula kazi yake vizuri. Wanjala (2012) anasema kuwa tafsiri ni mchakato wa uhawilishaji wa ujumbe katikamaandishi pamoja na uamilifu wake,

kutoka katika lugha chanzi hadi lugha lengwa kwa mujibu wa isimu, muktadha na utamaduni wa lugha zote mbili. Hivyo, mtafsiri huyu aliitumia mbinu hii ili tafsiri yake iweze kuwa nzuri na iwafikie walengwa wake kama alivyokusudia. Jambo hili linathibitishwa katika beti zifuatazo:

*8. Now the New Year reviving old Desires
The thoughtful soul to solitude retires
Where the white Hand of Moses on the Bought
Puts out, and Jesus from the Ground suspire*

Mwaka Mpya hufufua
Tamaa za zamani
Roho inapojitia
Kwa fikira faraghani
Kwa mkono alitia
Musa uzima tawini
Na Isa alipumua
Faraja duniani

*48. You know my friends, with what a brave carouse
I made a second marriage in my house
Divorced old barren Reasons from my bed
And took the Daughter of the vine to spouse*

Marafiki mwaelewa
Kwangu karibuni hivi
Arusi niliandaa
Mpya kwa mwingi Ulevi
Hoja bila Manufaa
Nimwacha mwenye mvi
Binti Mzabibu kawa
Mke wangu sasa hivi

*73. Listen again. One Evening at the close
Of Ramazan, ere the better moon arose
In that old potter's shop I stood alone
With the clay population round in Rows*

Tena sikilizeni
Siku moja jioni
Mwisho wa Ramadhani
Mfungomosi jirani
Kwa Mfinyanzi dukani
Nilikuwa pweke ndani
Watu wa Udongo ndani
Walisimama Safuni

Beti hizo zinazungumzia masuala ya kidini katika muktadha wa dini ya Kikristo ikioneshwa namna Yesu anavyoelezwa kama chanzo cha uhai. Pia, katika ubeti wa pili kunazungumziwa mambo ya harusi na namna mtu alivyofunga ndoa mara mbili na katika ubeti wa mwisho anazungumzia mambo ya mwezi wa ramadhani na mfungo mosi katika maudhui ya dini ya Kiislamu.

Mtafsiri Edward FitzGerald, wakati anatafsiri, alizingatia utamaduni wa jamii ya lugha lengwa ndiyo maana baadhi ya maneno, tunagundua kuwa aliamua kuyaweka hivyo ili yaendane na utamaduni wa Waingereza ikiwamo imani yake ya Kikristo. Mbinu ya kutafsiri kwa kuzingatia utamaduni hutumiwa na watafsiri ili kuwezesha jamii ya lugha lengwa kula kazi husika kwa muonjo na uzito uleule wa lugha chanzi. Kwa mfano, katika ubeti huo wa kwanza ametumia neno ‘*Jesus*’ ambalo hutumiwa na watu wenye imani ya Kikristo. Jina hilo, kwa imani ya Waislamu hutumika kama ‘Isa’. Hivyo, yeye aliamua kutumia jina hilo kwa mtindo huo kulingana na utamaduni wa jamii ya lugha lengwa. Vilevile, tukichunguza ubeti wa pili tunaona kuna maneno ‘*Second Marriage*’ na ‘*Divorced*’ ambayo yanasawiri utamaduni wa Kiingereza. Kwa mujibu wa utamaduni wao, ndoa huvunjika kwa kutoa talaka na taratibu za kisheria za kuachana huzingatiwa. Hivyo, mtu anapooa kwa mara nyingine kwa mujibu wa utamaduni wa Waingereza anakuwa ameo kwa mara ya pili. Neno jingine tunalionga katika ubeti wa tatu ni ‘*Better moon.*’ Shaaban Robert anatafsiri neno hili kuwa ni ‘mfungomosi’. Dhana hii inatupa mwanga kuwa Edward FitzGerald alilitafsiri hivyo kulingana na utamaduni wa jamii anayoitafsiria ili iweze kumwelewa.

Naye, Shaaban Robert katika kutafsiri utenzi huu alizingatia utamaduni wa jamii anayoitafsiria. Jamii ya Shaaban Robert ni ya Waswahili na isitoshe alikuwa na

itikadi ya Kiislamu. Resani² anaona kuwa katika, hali ya kawaida, mtafsiri hawezi kuepuka kuzingatia utamaduni wa jamii anayoitafsiria. Hii ni kwa kuwa lugha hubeba mambo mengi ya kiutamaduni; na isitoshe, lugha yenyewe ni sehemu ya utamaduni wa jamii husika. Mawazo haya yanaungwa mkono na Gromova (2004), Aziz (1982) na Sharififar (2007) wanapoeleza kuwa utamaduni wa lugha lengwa ni muhimu ukazingatiwa ili kuifanya tafsiri iwe na ladha kama ilivyo katika matini chanzi. Kwa mantiki hiyo, Shabaan Robert alitafsiri kwa kuzingati tamaduni za Waswahili, ikiwamo itikadi yake ya Kiislamu kama ilivyo asili ya utenzi wenyewe. Beti zifuatazo zinadhihirisha hili:

43. L.C. *You know, my friends, with what a brave carouse
I made a second marriage in my house
Divorced old barren Reason from my bed
And took the Daughter of the vine to spouse*

L.L. Marafiki mwaelewa
Kwangu karibuni hivi
Arusi niliandaa
Mpya kwa mwingi Ulevi
Hoja Bila Manufaa
Nimemwacha mwenye mvi
Binti Mzabibu kawa
Mke wangu sasa hivi

73. L.C. *Listen again. One Evening at the close
Of Ramazan, ere the better moon arose
In that old potter's shop I stood alone
With the clay population round in Rows*

L.L. Tena sikilizeni
Siku moja jioni
Mwisho wa Ramadhani
Mfungomosi jirani
Kwa mfinyanzi dukani
Nilikuwa pweke ndani
Watu wa Udongo ndani
Walisimama safuni

² Mahojiano yalifanyika kati ya mtafiti na Dkt. Mnata Resani wa Chuo kikuu cha Dodoma Tar. 14/02/2018. Huyu ni mtaalamu wa mambo ya isimu na ukalimani na anasomesha katika chuo hiki.

63. L.C. *And this I know: Whether the one True Light
Kindle to Love, or wrath- Consume me quite
On Gimpse of it within the Tavern Caught
Better than in the Temple lost outright*

L.L. Mimi naelewa kuwa
Nuru moja ya kweli
Mapenzi inayotia
Au Ghadhabu kudhili
Kuiona afadhali Kuliko ikipotea
Katika hekalu hili

Tukichunguza kwa makini beti hizo, na namna Shaaban Robert alivyotafsiri, tunagundua kuwa, alizingatia utamaduni wake wa Kiswahili na itikadi yake ya dini ya Kiislamu. Utafiti huu umegundua kuwa jambo hili lilisaidia kufikisha ujumbe kwa walengwa wake; na kuwafanya waile kazi yake kwa utamu uleule. Kwa mfano, tukichunguza ubeti huo wa kwanza na tafsiri yake, Edward FitzGerald anatumia neno ‘*second marriage*’ ambapo katika kutafsiri Shaaban Robert ametaja tu ‘Arusi’. Hii kwa utamaduni wa Waswahili, neno ndoa lina maana ya tendo zima la watu kuoana ambapo arusi ni sherehe ya ndoa. Kwa Waingereza arusi na ndoa yote yanabebwa na neno ‘*marriage*’. Neno jingine katika ubeti huu ni ‘*Divorced*’ likiwa na maana ya mtalaka au talaka. Hata hivyo, Shaaban Robert alipotafsiri anatumia neno ‘nimemwacha’. Kwa mujibu wa utamaduni wa Waswahili mke na mume hawafuati taratibu ndefu za kisheria katika kuachana kama ilivyo kwa utamaduni wa Waingereza. Ingawa kwa sasa mambo yameanza kubadilika kidogo na Waswahili nao wameanza kuachana kwa kufuata taratibu za kisheria tofauti na kipindi wakati Shaaban Robert anatafsiri utenzi huu. Shaaban Robert anatafsiri kwa namna hiyo kwa sababu alizingatia utamaduni wa Waswahili wa wakati huo.

4.3.2.4 Uzingatizi wa Mazingira

TUKI (1981) wanasema kuwa mazingira ni jumla ya mambo yote yanayomzunguka kiumbe katika maisha yake. Kwa hiyo, kila tunachokiona katika maisha ni mazingira yetu. Mazingira huweza kuundwa na vitu mbalimbali, vinaweza kuwa vya asili kama vile misitu, maziwa, mito, bahari na milima au visivyo vya asili kama vile barabara, majengo, mabwawa na misitu ya kupandwa. Mungai (2005) anaposema kuwa, tafsiri yeyote ile huhitaji kuzingatia elementi za kimazingira za wasomaji kabla ya kuamua ni mchakato gani utakaofuatwa katika kutafsiri. Mazingira haya ni pamoja na umri, tabia za wasomaji na aina za wasomaji pamoja na mazingira ya kijiografia maana baadhi ya msamiati katika lugha hupatikana kulingana na mazingira yanayoizunguka jamii. Kwa hiyo, watafsiri hawa walitafsiri kwa kuzingatia mazingira ya jamii wanazozitafsiria. Kwa mfano, Edward FitzGerald alitafsiri kwa kuzingatia mazingira ya jamii yake ya Waingereza. Mazingira ya Ulaya na Mashariki ya Kati kwa kiasi fulani hayafanani. Hivyo, katika tafsiri yake tunazona tofauti za kimazingira ambazo zimemfanya mtafsiri huyu atafsiri kwa mwelekeo tuonano. Beti zifuatazo zinathibitisha hili:

9. *Morning a thousand Roses brings, you say
Yes, but where leaves the Rose of Yesterday?
And this first summer month that brings the Rose
Shall take Jamshyd and Kaikobad away*

Siku ikipambazuka
Elfu yanachanua
Elfu hutawanyika
Na kupotea maua
Msimu ukifika
Wa Waridi kuchanua
Jamshyd atashika
Na Kaikobad njia

15. *Look to the Rose that blows about us – Lo
Laughing ‘she says’ into the World I blow
At once the silken Tassel of my Purse
Tear, and its Treasure on the Garden throw*

Tazameni kawaida
Waridi lichanuapo
Nafurahi kila muda
Husema pale lilipo
Wakati langu shada
Chini liangukapo
Hutawanya faida
Hazina mahali hapo

*29. I sometimes think that never blows so red
The Rose as where some buried Caesar bled
That every Hyacinth the Garden wears
Dropt in its Lap from some once lovely Head*

Katika yangu fuadi
Pengine ninafikiri
Huchanua Waridi
Kwa damu ya Kaizari
Ilipomwagwa zaidi
Tena kila ua zuri
Latoka hapana budi
Vinywani mwa mashuhuri

*32. Lo! Some we loved, the Loveliest and best
That time and Fate of all their vintage prest
Have drunk their cup a Round or two before
And one by one crept silently to Rest*

Kumbe watu tependao
Wapenzi walio bora
Katika Maisha yao
Na Ajali kila mara
Vuno la Zabibu zao
Walikunywa kwa duara
Kisha wakaenda zao
Kupumzika Ahera.

Beti hizo zinaongelea upendo kwa kuulinganisha na maua ya waridi, ambayo kwa utamaduni wa Kiingereza ni maua yenye thamani kubwa na yanaonesha upendo wa hali ya juu kwa mwanamke. Tukiangalia beti hizo tunaona kuwa Edward FitzGerald alitafsiri kwa kuzingatia mazingira ya Ulaya. Hii ni kwa sababu kuna baadhi ya maneno, kwa asili yake sio ya Kiajemi au yenye asili ya Mashariki ya Kati bali ni ya Ulaya. Kwa mazingira ya Ulaya, maua yenye thamani sana na yanayooneshwa upendo wa hali ya juu ni maua ya waridi (*rose*). Maua haya yanathamani kubwa kwa

utamaduni wa Waingereza kiasi cha kuwekwa hadi kwenye ngao ya taifa. Jambo hili linathibitishwa na Robertson (2008) anapoyaelezea maua haya na thamani yake kwa Waingereza. Anasema:

English rose is description, associated with English culture, that may be applied to a naturally attractive woman or girl of traditionally fair complexion who is from or is associated with England.

Maua ya waridi yanahusishwa na utamaduni wa Waingereza ambapo huweza kutumiwa kama mvuto wa asili kwa mwanamke au msichana wa kitamaduni mwenye ngozi nyororo ambaye anatoka au ana nasaba na Uingereza (Tafsiri ya Mtafiti). Robertson (khj) anasema kuwa maua haya yana historia ndefu katika nchi ya Uingereza anaendelea kulielezea jambo hili kuhusiana na maua ya waridi na utamaduni wa Waingereza kwa jinsi wanavyoathamini maua ya waridi. Anasema:

The Tudor rose, which is known more commonly as the red rose, is the natural flower of England. Whilst the red rose is therefore, used in various ways to represent England, it is in fact the traditional flower of Lancashire, which is a country in the North west of the Country.

Ua la waridi ambalo kwa kawaida linajulikana kama waridi jekundu ni ua la asili la Uingereza. Waridi jekundu linatumika katika namna mbalimbali kuwakilisha Uingereza, hili ni ua la kiutamaduni la Lancashire ambayo ni nchi iliyo Kaskazini Magharibi mwa nchi (Tafsiri ya Mtafiti).

Maelezo hayo yanatudhihirishia kuwa maua haya ni tofauti na maua ya kawaida kwa utamaduni wa Mwingereza. Neno hili ‘rose’ limejitokeza ubeti wa kwanza hadi wa tatu kuonesha msisitizo wa upendo na mapenzi ya juu sana kwa anayempenda. Pia tukichunguza ubeti wanne tutaona kuna neno ‘*Loveliest*’ neno hili nalo katika utamaduni wa Kiingereza linaonesha mapenzi ya juu zaidi ambapo katika lugha ya Kiswahili Shaaban Robert alitafsiri kama ‘wapenzi walio bora’ kitu ambacho ni tofauti na kile alichokuwa anamaanisha Edward FitzGerald. Kwa upande wa Shaaban Robert naye alipotafsirializingatia mazingira ya jamii ya lugha lengwa. Faiq (2004) anazungumzia changamoto zinazojitokeza katika kutafsiri matini za

kifasihi kuwa ni tofauti za kimazingira ambapo anashauri mtafsiri atafute visawe vinavyopatikana katika mazingira husika na viwe vinavyofanana kimaudhui na matini lengwa. Shaaban Robert naye alitumia mbinu hii. Kwa kuwa, mazingira ya Waingereza na mazingira ya Waswahili yanatofautiana, ilimbidi kuunda baadhi ya beti upya au kutoa baadhi ya maneno ili yaendane na mazingira ya Waswahili aliowatafsiria. Beti hapa chini zinathibitisha hili:

36. L.C. *I think the vessel, that with fugitive
Articulation answer'd, once did live
And Merry- make, and the cold Lip I kiss'd
How many kisses might it take and give*

L.L. Kwa tamko la kupita
Chombo kilichosema
Kuishi kilipata
Na kufurahi lazima
Kubusu ningalipata
Mdomo bila uzima
Faraja ungeleta
Ngapi na taathima!

55. L.C. *While the Rose blows along the River Brink
With old Khayyam and ruby vintage drink
And when the Angel with his darker Draught
Draws up to Thee- take that, and do not shrink*

L.L. Waridi lipepeapo
Penye mto ukingoni
Na Khayyam akiwapo
Divai bora kunyweni
Malaika aletapo
Kunywa kwake kwa fumboni
Msijikunje mlipo
Vivyo hivyo kunyweni

62. L. C. *And that inverted Bowl we call the sky
Where under Crawling coop't we live and die
Lift not thy hands to it for help- for it
Rolls importently on as Thou or I*

L.L. Bakuli katika hewa
Tuitalo Samawati
Chini yake twatambaa
Tukapatwa na mauti
Mikono kuliinulia
Yenu kwa dua sakiti
Mbinu hufingiria
Kama sisi umati

Mazingira ya Waswahili yanatofautiana na ya Waingereza. Kwa sababu hiyo, Shaaban Robert baadhi ya maneno ya Kiingereza aliyadondosha. Kwa mfano, katika ubeti wa kwanza kuna baadhi ya maneno aliamua kuyaacha kabisa na kuweka maneno yake. Kwenye ubeti wa pili kuna kifungu cha maneno '*Angel with his darker Draught*' yeye anatafsiri kama 'malaika aletapo'. Tunaaamini kuwa, kama angeamua kutafsiri kama maneno yalivyo ingemletea shida kueleweka. Pia, katika ubeti wa tatu kuna neno '*sky*' yeye amelitafsiri kama 'samawati'. Kwa sababu hiyo, aliamua kuweka maneno yanayoendana na mazingira ya Waswahili ili aweze kueleweka zaidi.

4.4 Kufanana na Kutofautiana kwa Tafsiri Mbili za Utenzi wa Omar Khayyam

Lengo letu la pili lilikuwa ni kulinganisha na kulinganua tafsiri mbili za *Utenzi wa Omar Khayyam* ile ya Kiingereza ya Edward FitzGerald na ile ya Kiswahili ya Shaaban Robert. Ponera (2014) anasema kulinganisha ni kufanya tathmini ya vitu viwili au zaidi ili kujua ubora, kufanana na kutofautiana kwavyo. Naye, Wamitila (2003) anasema ulinganisho wa fasihi ni kuchunguza, kuchambua na kueleza sifa za mfanano zilizopo katika matini ya fasihi. Pia, anasema kuwa ulinganuzi ni kuchunguza, kuchambua na kuonesha sifa zinazotofautiana baina ya matini mbili au zaidi za kifasihi. Kwa maana hiyo, hapa tunaangalia namna matini hizi zinavyofanana na kutofautiana. Baada ya kuzichunguza tafsiri hizi mbili, mambo yafuatayo yalijitokeza tukianza na kufanana kisha kutofautiana.

4.4.1 Kufanana kwa Tafsiri za Utenzi wa Omar Khayyam

Tafsiri mbili za utenzi huu, kama ilivyoelezwa hapo mwanzo kuwa zilifanywa na watu wawili wenye tofauti za lugha, tamaduni na mazingira yao. Utafiti umegundua kuwa, pamoja na tofauti hizo tafsiri hizi zinafanana katika mambo yafuatayo:

4.4.1.1 Kufanana katika Mbinu za Kufanya Tafsiri

Watafsiri hawa wanafanana katika baadhi ya mbinu walizotumia kufanya tafsiri zao. Kama ilivyoelezwa hapo awali kuwa kuna mbinu mbalimbali walizotumia watafsiri hawa katika kufanya tafsiri. Katika kufanana, wote walitumia mbinu ya uzingatizi wa mazingira, uzingatizi wa utamaduni wa jamii unayoitafsiria, uzingatizi wa maana au maudhui yaliyomo katika matini chanzi na uzingatizi wa umbo la matini chanzi.

4.4.1.2 Kufanana wa Kimaudhui

Tafsiri ya Edward FitzGerald na Shaaban Robert zinafanana kimaudhui kwani ukichunguza baadhi ya beti katika utenzi huu, maudhui ya matini chanzi na yale ya matini lengwa yanafanana ijapokuwa mfanano huo hauwezi kuwa wa asilimia miamoja. Kwa mfano, beti zifuatazo maudhui yake yanafanana.

33. L.C. *There was the Door to which I found no Key
There was the Veil through which I could not see
Some little talk awhile of Me and Thee
There was – and then no more of Thee and Me*

L.L. Mlango ulitokea
Sikuona Ufunguo
Nikaliona Pazia
Lisilopenya Upeo
Kidogo tukiongea
Mimi nawe maongeo
Mimi nawe tusemao

34. L.C. *Then to the rolling Heav'n itself I cried
Asking, What Lamp had Destiny to guide
Her little Children stumbling in the Dark?
And – A blind Understanding! Heav'n replied*

L.L. Ndipo nilpoanza
Ukelele Mbinguni
Kusudi kuiuliza
Ajali Taa gani
Wanawe kuwaongoza
Wasianguke Gizani?
Na Mbingu ikaeleza
Elimu ya ujingani

30. L.C. *Then to the Lip of poor earthen Urn
I lean'd the secret Well of Life to learn
And Lip to Lip it murmur'd – While you live
Drink! – for, once dead, you never shall return*

L.L. Nipokizohalisha
Kinywa katika Dunia
Kisima cha maisha
Siri yake kuijua
Kinywa kilijisemesha
Mzima unapokuwa
Kunywa! Kwa sababu yakiisha
Maisha hutarejea

Kuna kufanana kwa maudhui au maana ya beti hizi, ijapokuwa si kwa asilimia miamoja. Kwa kiasi fulani, mguso na muonjo wa matini chanzi unausikia pia katika matini lengwa. Hii ni kwa kuwa lengo la tafsiri kwa misingi ya nadharia ya ulinganifu ni kufikia usambamba wa kimaudhui kati ya matini chanzi na matini lengwa.

4.4.1.3 Kufanana katika Mtindo (Kuzingatia Vina na Mizani)

Utunzi wa mashairi upo katika mikondo mikuu miwili ya mtindo wa uandishi wake. Kuna mtindo wa kimapokeo wa kufuata vina na mizani na kuna mtindo wa kisasa usiozingatia vina na mizani. Utafiti huu umegundua kuwa, watafsiri hawawanafanana katika mtindo wao; kwani, walipotafsiri walizingatia vina na mizani katika kila beti. Jambo hili ni matokeo ya wote wawili kuwa ni waumini wa mashairi ya mtindo wa kimapokeo. Utafiti umebaini kuwa, watafsiri hawa wanafanana katika utunzi wao kwa kuwa hufuata urari wa vina na mizani.

Tukiangalia mashairi ya Edward FietzGerald tunaona kuwa yanazingatia vina na mizani. Hali kadhalika, mashairi ya Shaaban Robert nayo yana mtindo huo. Kwa hiyo, katika tafsiri hizi ilikuwa ni lazima wafanane tu katika mtindo maana wanamitazamo sawa katika hili. Beti zifuatazo zinathibitisha hili.

27. L.C. *Why, all the Saints and Sages who discuss'd
Of the Two Worlds so learnedly, are thrust
Like foolish Prophets forth, their Works to Scorn
Are scatter'd and their Mouths are stop with Dust*

L.L. Mbona Wenye hekima
Wote na Mawalii
Mno waliosema
Pepo na Dunia hii
Wametupwa kama
Wajinga Manabii
Vinywa vyao vimekoma
Kwa vumbi hawafunui?

21. L.C. *Oh, come with old Khayyam, and leave the Wise
To talk, one thing is certain, that Life flies
One thing is certain and the Rest is Lies
The Flower that once has blown forever dies*

L.L. Aha, mfuateni Khayyam
Waacheni Wenye hekima
Jambo moja maalum
Kuwa maisha huhama
Jambo moja maalum
Mengine yote si tama
Ua lililodumu
Lifapo hufa daima

45. L.C. *Myself when young did eagerly frequent
Doctor and Saint, and heard great Argument
About it and about, but evermore
Came out by the same Door as in I went*

L.L. Mara nyingi kwa bidii
Nilipokuwa kijana
Mashehe na Mawalii
Hoja tulifanyiana
Lakini sikukinai
Daima nilipoona
Nikija kwa njia hii
Narudi kwa njia hii tena.

Tukichunguza kwa makini beti hizo hapo juu tunaona kuwa watafsiri hawa walizingatia mtindo wa kufuata urari wa vina na mizani. Kwa mfano, ubeti wa kwanza lugha chanzi anaishia na sauti ‘i’ na kwa upande wa lugha lengwa anaishia sauti ‘a’ na ‘i’. Pia, tukiangalia ubeti wa tatu lugha chanzi anaishia na sauti ‘z’ na lugha lengwa yeye anaishia na ‘m’ na ‘a’ pia ubeti wa tatu lugha chanzi ameishia na sauti ‘i’ na lugha lengwa ameishia na sauti ‘i’ na ‘a’. Kwa maana hiyo, watafsiri hawa wanafanana katika kuzingatia urari wa vina na mizani.

4.4.1.4 Kufanana Katika Nia ya Kutafsiria Jamii Zao

Tukiwaangalia watafsiri wenyewe, tunagundua kufanana kwao katika nia njema ya kuitafsiria jamii yao. Edward FitzGerald alikuwa na nia njema ya kuitafsiria jamii yake ya Waingereza kuwafanya waile kazi ya Omar Khayyam kutoka lugha ya Kiajemi akaileta katika lugha ya Kiingereza. Nia hii njema tunaiona pia kwa Shaaban Robert alipoamua kuitafsiri kazi hii kutoka lugha ya Kiingereza na kuileta katika lugha ya Kiswahili ili, Waswahili nao wapate fursa ya kuifaidi kazi hii. Jambo hili tunalionga katika utangulizi wa tafsiri hii, Robert (1973) akimnukuu Ishawood anaposema:

Nimekupelekea kazi hii kwa kujua kwangu ulivyo mwanachama wa mashairi. Nimeona kuwa hutakosa kukifasiri na kuweza kujipatia kujua maana ya maneno kadhaa wa kadhaa tutumiayo hapa Afrika Mashariki ukipata kukisoma barabara hutakosa kufanya neno la kufaa, nikujuavyo wewe u – mwelewa wa mashairi basi utanza kufasiri na kuyapanga mashairi kadri ya ustadi wako kama huyo alivyofanya huyo Bwana Edward FitzGerald alivyotoa katika Kiajemi yakawa ya Kiingereza (uk 104).

Maelezo hayo yanadhihirisha kuwa nia za watu hawa za kuzifanya jamii zao waipate kazi hii kwa lugha yao zilikuwa zinafanana. Pia, inaonekana Ishawood alikuwa anamfahamu vizuri Shaaban Robert kuwa ni mtu mahiri katika ushairi hivyo hakuwa na shaka kuwa kazi hii itafanyika vizuri pasi na shaka yoyote. Kufanana kwa nia hii

mioyoni mwa washairi hawa kunadhihirishwa pia na mwendelezo wa maneno haya ya Ishawood baada ya Shaaban Robert kumaliza kutafsiri mashairi haya na kumrudishia kitabu chake na mashairi yaliyotafsiriwa. Robert (1973) analizungumzia hili akimnukuu Ishawood anasema:

Nimependezwa sana kwa kazi hii niliyokupelekea ulivyoichukua kwa moyo wa furaha na juhudi hata ikapata kuwa hivi. Mimi niliona vyema elimu ya mtungaji huyo Omar Khayyam wa Ajemi ifahamike na watungaji wa pande za Afrika Mashariki pia. Basi kazi uliyoifanya itawafaidia jamaa na rafiki za wenzako wengi watakaopata kuiona. Hivyo watapata kutambua kuwa utungaji wa mashairi upo mahali pengi (uk 104).

Maneno hayo yalituonesha namna ambavyo kazi hii ilitafsiriwa ili iweze kuwafikia na watu wa Afrika Mashariki. Mwandishi anaonesha kuwa kama ilivyokuwa kwa mtafsiri Edward FitzGerald ya kuufanya utenzi huu ujulikane kwa Waingereza pia ni vyema utenzi huu ukajulikana kwa watu wa Afrika Mashariki. Wazo hili la kufanana kwa nia za watafsiri linaungwa mkono na Resani (khj) anabainisha kuwa watafsiri hawa wanafanana katika nia yao ya kutafsiria jamii zao kazi za lugha tofauti ili jamii zao ziweze kufaidi kazi hizo. Anaona kuwa jambo hili ni la kwanza kabisa katika kufanana kisha mambo mengine yanafuata.

4.4.2 Kutofautiana kwa Tafsiri Hizi

Wamitila (2003) anasema kuwa, ulinganuzi ni kuchunguza, kuchambua na kuonesha sifa zinazotofautiana baina ya matini mbili au zaidi za kifasihi. Kwa sababu hiyo, mbali na kufanana kwa tafsiri hizi pia, zinatofautiana katika mambo mbalimbali. Mambo hayo yanayotofautiana katika tafsiri hizi kama yalivyopatikana katika utafiti huu ni haya yafuatayo:

4.4.2.1 Tofauti za Kiutamaduni

Utamaduni wa Waingereza na utamaduni wa Waswahili unatofautiana kwa kiasi kikubwa. Kwa hiyo, wakati watafsiri hawa wanafanya kazi yao ya kutafsiri kila mmoja alizingatia utamaduni wa jamii anayoitafsiria. Edward FitzGerald alizingatia utamaduni wa Kiingereza na Shaaban Robert alizingatia utamaduni wa Waswahili. Ponera (2014) akifafanua neno hili utamaduni anasema kuwa ni dhana ya jumla inayobeba dhana nyinginezo kama vile matumizi ya lugha, mitazamo ya kijamii, matumizi ya mavazi, misingi ya kimaisha ya jamii husika na sanaa za kijadi. Pia, kwenye utamaduni tunaliona suala la itikadi ya dini likijitokeza ambapo Edward FitzGerald ni Mkristo na Shaaban Robert ni Mwislamu. Beti zifuatazo zinathibitisha jambo hili:

8. *L.C. Now the New Year reviving old Desires
The thoughtful Soul to Solitude retires
Where the White Hand of Moses on the Bought
Puts out, and Jesus from the Ground suspires*

L.L. Mwaka mpya hufufua
Tamaa za zamani
Roho inapojitia
Kwa fikira faraghani
Kwa mkono alitia
Musa uzima tawini
Na Isa alipumua
Faraja duniani

Tukiangalia ubeti huo kunajitokeza suala la tofauti za kiutamaduni kulingana na itikadi za kidini. Hapa tunamuona Edward FitzGerald anataja jina ‘Jesus’ kulingana na imani yake ya Kikristo lakini anapokuja Shaaban Robert kutafsiri yeye anataja jina ‘Isa’ kulingana na itikadi ya imani yake ya dini ya Kiislamu hizi ni tofauti za kiutamaduni katika misingi ya imani ya dini. Hebu tuchunguze tena beti zifuatazo kuhusiana na hoja hii:

9. L.C. *Morning a thousand Roses brings, you say
Yes, but where leaves the Rose of Yesterday?
And this first summer Month that bring the Rose
Shall take Jamshyd and Kaikobad away*

L.L .Siku ikipambazuka
 Elfu yanachanua
 Elfu hutawanyika
 Na kupotea maua
 Msimu ukifika
 Wa waridi kuchanua
 Jamshyd atashika
 Na Kaikobad njia

Tukichunguza beti hizo tunagundua tofauti za kiutamaduni zilizosababisha tofauti katika kutafsiri. Kwa mfano, katika mshororo wa kwanza Edward FitzGerald anafananisha upendo na maua ya waridi (*rose*) Maua haya kwa utamaduni wa Mwingereza ni zaidi ya maua ya kawaida. Hii ni kwa sababu yanatumiwa ili kuonesha upendo wa hali ya juu. Shaaban Robert alipokuja kutafsiri kutokana na utamaduni wa Waswahili kuhusu maua, Waswahili maua ni maua tu na yote mara nyingi yanawekwa kwenye daraja moja. Pia, thamani ya maua kwa Waswahili ni ya aina ileile; ndiyo maana yeye katika mshororo huo anataja neno ‘maua’ tu bila kuonesha upekee tunaouona kwa Edward FitzGerald. Beti zingine zinazoonisha jambo hili la utamaduni ni hizi zifuatazo:

73. L.C. *Listen again. One Evening at the close
Of Ramazan, ere the better moon orese
In that old potter's shop I stood alone
With the clay population round in Rows*

L.L. Tena sikilizeni
 Siku moja jioni
 Mwisho wa Ramadhani
 Mfungomosi jirani
 Kwa mfinyanzi dukani
 Nilikuwa pweke ndani
 Watu wa Udongo ndani
 Walisimama safuni

Tukichunguza tena kwa makini beti hizi, hasa mshororo wa pili katika lugha ya Kiingereza, tunaona Edward FitzGerald anasema ‘*the better moon arose*’ akimaanisha mwezi mtukufu kuandama. Maneno haya yalipokuja kutafsiri na Shaaban Robert akasema ‘mfungomosi jirani’. Hizi ni tofauti za kiutamaduni zilizozingatiwa na Edward FitzGerald ambapo aliona kuwa akitafsiri hivyo jamii anayotafsiria wataamwelewa. Dhana hii ilipokuja kutafsiriwa na Shaaban Robert kulingana na weredi mkubwa aliokuwa nao katika masuala ya dini ya Kiislamu, aliamua kutafsiri hivyo kwani baada ya Mfungo wa Ramadhani unaofuata huwa ni mfungomosi.

4.4.2.2 Tofauti za Kimazingira

Msamiati mwingi wa lugha yoyote hutokana na mazingira anamoishi mwanadamu. Jambo hili limekuwa likiwaletaka shida sana watafsiri wa kazi za fasihi kwani kunabaadhi ya msamiati unaopatikana katika lugha chanzi unaweza usipate kabisa kisawe chake katika lugha lengwa. Jambo hili limetazamwa na Mwansoko³ anaposema:

Unapokuwa unafanya tafsiri, kuzingatia mazingira ya jamii unayotafsiria ni jambo la lazima, kwani maneno mengi katika lugha au msamiati mwingi wa lugha umezaliwa kutokana na mazingira. Tunaweza kusema lugha yoyote imetokana na mazingira. Hivyo basi, utofauti wa mazingira ni chanzo kikuu cha mwachano wa tafsiri hizi maana ndani ya mazingira utapata isimu ya lugha husika, mila na desturi, pamoja na utamaduni wa jamii husika.

Tukichunguza tafsiri hizi mbili za *Utenzi wa Omar Khayyam* tunagundua tofauti za kimazingira zilipelekea mtafsiri kutafsiri kama alivyotafsiri kwa baadhi ya maneno kuyaacha na kuweka visawe vipya. Beti zifuatazo zinaonesha hili:

³ Mahojiano yalifanyika kati ya Mtafiti na Prof. Mwansoko wa Chuo Kikuu cha TEKU Tar. 08/02/2018. Huyu ni mtaalamu wa masuala ya tafsiri na anasomesha katika chuo hiki.

34. L.C. *And this I know: Whether the one True Light
Kindle to Love, or wrath- Consume me quite
On Gimpse of it within the Tavern Caught
Better than in the Temple lost outright*

L.L. Mimi naelewa kuwa
Nuru moja ya kweli
Mapenzi inayotia
Au Ghadhabu kudhili
Ndani ya Mkahawa
Kuiona afadhali
Kuliko ikipotea
Katika hekalu hili

Utafiti huu umegundua kuwa, Shaaban Robert kuna baadhi ya maneno aliyadondosha baada ya kukosa visawe vya maneno ambavyo vingelea mguso sawa na ule wa lugha chanzi. Kwa mfano, maneno ‘*Consume me quite*’ Shaaban Robert hakuyatafsiri kabisa. Jambo hili linaendelea kudhihirika katika beti zifuatazo:

31. L. C. *And that inverted Bowl we call the sky
Where under Crawling coop't we live and die
Lift not thy hands to it for help- for it
Rolls importently on as Thou or I*

L.L. Bakuli katika hewa
Tuitalo Samawati
Chini yake twatambaa
Tukapatwa na mauti
Mikono kuliinulia
Yenu kwa dua sakiti
Mbinu hufingiria
Kama sisi umati

Tukiangalia ubeti huo hasa mshororo wa kwanza tunaona baadhi ya maneno kama ‘*inverted*’ na neno ‘*sky*’ kwenye tafsiri ya Shaaban Robert yeye ameweka maneno ‘hewa’ na neno ‘Samawati’ maneno ambayo hayaendani na maana halisi katika lugha chanzi. Mantiki hii inajengwa na mazingira ya jamii aliyokuwa anaitafsiria na hali ya kulazimika kuweka visawe vipya kulingana na jamii anayoitafsiria. Jambo hili tunaendelea kuliona tena katika beti zifuatazo:

36. L.C *I think the vessel, that with fugitive
Articulation answer'd, once did live
And Merry- make, and the cold Lip I kiss'd
How many kisses might it take and give*

L.L. Kwa tamko la kupita
Chombo kilichosema
Kuishi kilipata
Na kufurahi lazima
Kubusu ningalipata
Mdomo bila uzima
Faraja ungeleta
Ngapi na taathima!

Tukiuangalia kwa makini ubeti huu tunagundua kuwa Shaaban Robert aliacha maneno mengi tu kuyatafsiri katika ubeti huu. Sababu kubwa iliyomsukuma kuacha ni tofauti za kimazingira zilizopo ili kuleta maudhui yaliyokusudiwa. Karibia ubeti wote ulivyo katika lugha chanzi ni tofauti na ulivyo katika lugha lengwa.

4.4.2.3 Tofauti za Kiisimu

Kila lugha ina isimu yake, isimu ya lugha ya Kiingereza ni tofauti na isimu ya lugha ya Kiswahili. Katika tafsiri hizi mbili za *Utenzi wa Omar Khayyam* tunaona tofauti za kiisimu kati ya lugha ya Kiingereza na lugha ya Kiswahili. Hii ni kwa sababu mpangilio wa maneno katika lugha ya Kiingereza ni tofauti na mpangilio wa maneno katika lugha ya Kiswahili. Beti zifuatazo zinathibitisha hili.

35. L.C. *Then to the Lip of this poor eathern urn
I learn'd the secret well of life to learn
And Lip to Lip it murmurd- while you live
Drink! - for, once dead you never shall return*

L.L. Nipokizoharisha
Kinywa katika Dunia
Kisima cha Maisha
Siri yake kuijua
Kinywa kilijisemesha
Mzima unapokuwa
Kunywa! Kwa sababu yakiisha
Maisha hutarejea.

Tukiangalia maneno aliyotumia Edward FitzGerald katika mshororo wa kwanza yapo kama maneno tisa ‘*Then to the Lip of this poor eathern urn*’ ambayo katika tafsiri ya Shaaban Robert yanabebwa na maneno manne tu ‘Nilipokizoharisha Kinywa katika Dunia’. Hii ni tofauti ya kiisimu inayojitokeza katika tafsiri hizi mbili za *Utenzi wa Omar Khayyam*, ambapo baadhi ya maneno katika lugha moja ni marefu mno au mafupi mno. Katika tafsiri hizi mbili, vipengele vya kufanana na kutofanana karibu viko sawa ijapokuwa utafiti huu umegundua kuwa kufanana kumechukua sehemu kubwa ya matini hizi kuliko kutofautiana kwake.

4.5 Sababu za Kuwapo kwa Mwachano wa Tafsiri Hizi za *Utenzi wa Omar Khayyam*

Lengo letu la tatu katika utafiti wetu lilikuwa ni kutathmini sababu za kuwepo kwa mwachano wa tafsiri mbili za *Utenzi wa Omar Khayyam*. Utafiti umekuja na matokeo yafuatayo kuhusiana na lengo hili:

4.5.1 Ugumu wa Kutafsiri Utanzu Husika

Wataalamu kama vile, Mshindo (2010), Ombaga (1986) na Makacha (2013) wanakubaliana kuwa, kutafsiri ushairi siyo jambo jepesi hata kidogo. Hii ni kazi ngumu inayohitaji umakini wa hali ya juu sana tofauti na tanzu zingine za fasihi. Newmark (1988) anasema kuwa ushairi ndiyo utanzu wa fasihi ulio mgumu zaidi kufasirika. Hii ni kwa sababu, kila neno katika ushairi lina maana na ushairi una mshindilio mkubwa wa mawazo. Naye, Mwansoko (2013) akishadidia hili, anasema kuwa katika ushairi neno na mstari licha ya kubeba maana lakini lina umuhimu mkubwa sana katika utanzu huu kuliko tanzu nyingine. Hii ni kwa sababu, licha ya kubeba maana za kawaida, neno pia hubeba sauti na milio kwa namna ya kimpangilio tofauti na tanzu zingine.

Maelezo hayo yanatuonesha ugumu uliopo katika kutafsiri ushairi, kwani kunahitaji uzingativu wa hali ya juu ili kazi ya mtafsiri huyu iweze kuwa na mguso sawa na matini chanzi. Utafiti umegundua kuwa matini chanzi ina beti 90 na matini lengwa ina beti 67. Mwachano huu wa idadi ya beti ulisababishwa na ugumu wa kutafsiri baadhi ya beti. Hivyo, Shaaban Robert kuamua kuziacha kabisa kuzitafsiri. Kwa mfano, hakutafsiri kabisa beti namba 8, 14, 38, 49, 50, 51, 52, 53, 54, 56, 57, 61, 64, 68, 69, 70, 82, 83, 84, 85, 86, 87, 88, 89 na 90.

Pia, utafiti umegundua kuwa beti katika tafsiri hizi hazifuatani kwa mtiririko uliomzuri kinamba. Jedwali lifuatalo linaonesha mpangilio wa beti na namna zilivyotafsiriwa.

Jedwali Na. 1 Mpangilio wa Beti Zilivyotafsiriwa

Na.	L.C. (Ubeti)	L.L. (Ubeti)	Na.	L.C. (Ubeti)	L.L. (Ubeti)
1.	1	1	33.	35	34
2.	2	2	34.	36	35
3.	3	3	35.	37	36
4.	4	4	36.	39	37
5.	5	5	37.	40	38
6.	6	6	38.	42	39
7.	7	7	39.	43	40
8.	9	8	40.	44	42
9.	10	9	41.	45	43
10.	11	10	42.	47	45
11.	12	11	43.	48	46
12.	13	12	44.	46	47
13.	15	13	45.	55	48
14.	16	14	46.	58	49
15.	17	15	47.	59	50
16.	18	16	48.	60	51
17.	19	17	49.	62	52
18.	20	18	50.	63	53
19.	21	19	51.	65	54
20.	22	20	52.	66	55
21.	23	21	53.	67	56
22.	24	22	54.	71	57
23.	25	23	55.	72	58
24.	26	24	56.	73	59
25.	27	25	57.	74	60
26.	28	26	58.	75	61
27.	29	27	59.	76	62
28.	30	28	60.	77	63
29.	31	29	61.	78	64
30.	32	31	62.	79	65
31.	33	32	63.	80	66
32.	34	33	64.	81	67

Chanzo: Utafiti (2018)

Jedwali, hapo juu linaonesha mchanganyo wa mpangilio wa beti kulingana na zilivyotafsiriwa kiasi kwamba tukichukua matini chanzi na matini lengwa tutaona zinaachana kwa idadi ya beti na mpangilio wake. Kutokana na kurukwa kwa baadhi ya beti katika kutafsiri, mtiririko wake haujaenda sawa. Katika mtiririko wa tafsiri ikiwa mtu hatakuwa makini katika kuchunguza anaweza kudhani kuwa tafsiri karibia yote imekosewa.

Jambo jingine ambalo utafiti umegundua Shaaban Robert alitunga beti mpya kabisa tatu, yaani ubeti wa 30, 41 na 44. Kwa hiyo, tukichukua idadi ya beti zilizomo katika matini lengwa 67, tukaongeza na beti ambazo hakuzitafsiri 26 kisha tukitoa beti tatu ambazo alitunga mpya kabisa, tunapata idadi ya beti 90 sawa na idadi ya matini chanzi ilivyo. Hii inaondoa mashaka yaliyokuwepo kuhusu uwiano wa idadi hasa ya beti kutoka matini chanzi na matini lengwa.

Mbinu hii ya kutunga beti mpya inashadadiwa na Makacha (2013) anaposema kuwa kutafsiri shairi kishairi kunampa fursa mshairi kuyapa maudhui aliyoyatafsiri ladha yake ya kisanaa. Hivyo basi, ni muhimu mtafsiri wa ushairi alitafsiri shairi kishairi.

4.5.2 Tofauti za Kiisimu

Isimu ya lugha hizi hailingani. Hivyo, tofauti hii ya kiisimu ilisababisha mwachano katika tafsiri hizi mbili. Kwa mfano, baadhi ya maneno kwenye lugha moja yanaweza kuwa marefu sana na katika lugha nyingine kuwa mafupi. Jambo hili lilisababisha baadhi ya beti kuwa na maneno mapya kabisa na baadhi ya mishororo kudondoshwa. Kwa mfano, beti zifuatazo zinathibitisha hili.

*7. L.C. Come, fill the Cup, and in the Five of Spring
The Winter Garment of Repentance fling
The Bird of Time has but a little way
To fly- and Lo! The Bird is on the Wing*

L.L. Njoo ujaze Kikombe
Huzuni yako ivue
Isikate kama wembe
Katika moto itie
Haya maisha ni chembe
Kama ndege mfanowe
Ghafla hii kumbe
Huruka kwa mabawaye

Tukichunguza kwa makini ubeti huu tunagundua kuwa mshororo wa pili wa lugha chanzi haujatafsiriwa katika lugha lengwa. Mtafsiri ameuondosha ubeti huo kwa sababu za kiisimu na sheria zinazotakiwa kufuatwa wakati wa kutunga mashairi, hasa kufuata mtindo wa vina na mizani. Beti zingine zinazothibitisha jambo hili ni hizi zifuatazo:

*22. L.C. Ah, my Beloved, fill the Cup that clears
To-day of past Regrets and future Fears
To-morrow? Why, Tomorrow I may be
Myself with Yesterday's Sev'n Thousand Years*

L.L. Aha, mpenzi wangu
Jaza bilauli hiyo
Initoe machungu
Ya zamani niwazayo
Tena iondoke kwangu
Hofu ya Kesho ijayo
Karne sabiini kwangu
Jana nitakuwa nayo

Tukichunguza lugha chanzi katika ubeti huu, mshororo wa pili Shaaban Robert hakuutafsiri kama ulivyo isipokuwa aliweka maneno yake. Hii ni kwa sababu awezekulinda vina na mizani bila kupoteza maana ya ubeti mzima.

4.5.3 Tofauti za Kiutamaduni

Kama ilivyoielezwa hapo mwanzo kuwa utamaduni unajumuisha mambo mengi ikiwamo jambo la imani ya dini. Itikadi za dini za watafsiri hawa zinatofautiana, Edward FitzGerald itikadi yake ni dini ya Kikristo na Shaaban Robert itikadi yake ni dini ya Kiislamu. Tofauti ya itikadi hizi zilisababisha mwachano wa tafsiri hizi

mbili, kwani kama ilivyoelezwa hapo mwanzo kuwa utenzi huu wa Omar Khayyam maudhui yake makuu ni ya kidini hasa dini ya Kiislamu. Hivyo, hata tafsiri za utenzi huu zina maudhui ya kidini lakini kutokana na utofauti wa itikadi za dini za watafsiri hawa kuna mwachano katika tafsiri zao. Chuachua (2011) anaeleza kuwa, itikadi ni mawazo fulani ambayo ni misingi ya nadharia za mifumo ya kisiasa, kiuchumi na kijamii. Hivyo, kwa tafsiri hii misingi hii siyo rahisi kubadilika na mara nyingi mtu ataelemea katika itikadi yake. Beti zifuatazo zinaonesha jambo hili:

73. L.C. *Listen again. One Evening at the close
Of Ramazan, ere the better moon arose
In that old potter's shop I stood alone
With the clay population round in Rows*

L.L. Tena sikilizeni
 Siku moja jioni
 Mwisho wa Ramadhani
 Mfungomosi jirani
 Kwa mfinyanzi dukani
 Nilikuwa pweke ndani
 Watu wa Udongo ndani
 Walisimama safuni

6. L.C *Now the New Year reviving old Desires
The thoughtful Soul to Solitude retires
Where the White Hand of Moses on the Bought
Puts out, and Jesus from the Ground suspires*

L.L. Mwaka mpya hufufua
 Tamaa za zamani
 Roho inapojitia
 Kwa fikira faraghani
 Kwa mkono alitia
 Musa uzima tawini
 Na Isa alipumua
 Faraja duniani

Tukichunguza kwa makini ubeti huu, hasa mshororo wa pili katika lugha ya Kiingereza tunaona kuwa Edward FitzGerald akisema ‘*the better moon arose*’ kwa maana ya mwezi mtukufu kuandama. Shaaban Robert alipotafsiri akasema ‘mfungomosi jirani’. Hizi ni tofauti za kiitikadi katika dini, kwa mantiki hii Edward

FitzGerald aliona akitafsiri hivyo jamii anayoitafsiria ya Wakristo watamwelewa kwa urahisi. Kwa upande mwingine, Shaaban Robert alipotafsiri kulingana na kuwa na ufahamu mkubwa katika masuala ya dini ya Kiislamu, aliamua kutafsiri hivyo kwa kuwa baada ya Mfungo wa Ramadhani unaofuata huwa ni mfungomosi. Jambo hili la tofauti za kiitikadi ya dini linajitokeza tena katika ubeti ufuatao:

6. L. C *Now the New Year reviving old Desires
The thoughtful Soul to Solitude retires
Where the White Hand of Moses on the Bought
Puts out, and Jesus from the Ground suspires*

L. L Mwaka mpya hufufua
 Tamaa za zamani
 Roho inapojitia
 Kwa fikira faraghani
 Kwa mkono alitia
 Musa uzima tawini
 Na Isa alipumua
 Faraja duniani

Tukichunguza maudhui ya ubeti huu, tunaona kuwa kutokana na tofauti za kiitikadi katika dini za watafsiri hawa, Edward FitzGerald alitumia jina ‘Jesus’ kulingana na itikadi yake ya dini ya Kikristo. Naye, Shaaban Robert alipokuja kutafsiri jina hilo yeye alitumia jina ‘Isa’ hii ni kutokana na itikadi ya dini yake ya Kiislamu. Mwachano huu umesababishwa na tofauti za kiutamaduni katika itikadi ya dini kwa watafsiri hawa Edward FitzGerald akiwa Mkristo na Shaaban Robert akiwa Muislamu. Beti zingine zinazoonisha jambo hili ni hizi zifuatazo:

24. L. C *And we, that now make merry in the Room
They left, and Summer dresses in new Bloom
Ourselves must we beneath the Couch of Earth
Descend, ourselves to make a Couch – for whom?*

L. L Na sisi tufurahio
 Sasa katika Chumba
 Walichokiacha wao
 Msimu mpya watamba
 Itatubidi kwa hiyo
 Tushuke chini kuchimba
 Ya nini malazi hayo
 Tushukayo kuyapamba?

Tukiuchunguza ubeti huo pia, tunaona tofauti za kiutamaduni katika jamii za Waswahili na Waingereza. Kwa mfano, katika lugha chanzi kuna maneno ‘*Summer dresses*’ ambayo yana maanisha mavazi maalumu kwa majira maalumu katika mwaka kwa Waingereza. Shaaban Robert alipotafsiri alitaja tu maneno ‘msimu mpya’ wala hakujishughulisha na neno mavazi. Katika utamaduni wa Waswahili hatuna mavazi maalumu kulingana na majira ya mwaka kama ilivyo kwa Waingereza.

4.5.4 Mihula Tofauti ya Nyakati

Ponera (2014) akielezea kipengele hiki, anasema kuwa, ni muda ambao kazi fulani au mtindo fulani wa sanaa ulijitokeza au kushamiri, anaendelea kusema kuwa vipengele mbalimbali vya kazi ya sanaa hubadilika kutokana na uwakati. Uwakati ni sababu mojawapo inayoweza kusababisha mwachano katika tafsiri, kwani kama tunavyojua lugha ina tabia ya kuzaliwa kukua na kufa. Hivyo, kama utapita muda mrefu sana tangu matini chanzi itolewe na tafsiri ya matini hiyo, ni wazi baadhi ya mambo yaliyo katika matini chanzi yatakuwa yameshafifia au kutoweka kabisa. Hata hivyo, jambo hili halijajidhihirisha sana katika tafsiri hizi. Hii ni kwa sababu utenzi huu umejikita sana katika mambo ya dini ambayo ni nadra sana kubadilika. Hoja ya mihula tofauti ya nyakati tunaiona katika ubeti ufuatao:

43. L.C. *You know, my friends, with what a brave carouse
I made a second marriage in my house
Divorced old barren Reason from my bed
And took the Daughter of the vine to spouse*

L.L. Marafiki mwaelewa
Kwangu karibuni hivi
Arusi niliandaa
Mpya kwa mwingi Ulevi
Hoja Bila Manufaa
Nimemwacha mwenye mvi
Binti Mzabibu kawa
Mke wangu sasa hivi

Hapa tuliangalia maneno mawili ambayo yanaonesha utofauti wa nyakati. Maneno hayo ni “*Divorced*” likiwa na maana ya talaka au mtalaka. Shaaban Robert alitafsiri kama “nimemwacha” maneno hayo hayana uzito kama aliomaanisha Edward FitzGerald kwani yeye anaonesha utaratibu unaotakiwa katika kuachana. Shaaban Robert alitafsiri hivyo kwani kipindi hicho Waswahili walikuwa wanaachana tu bila kufuata taratibu ndefu kama ilivyo sasa.

4.6 Muhtasari wa Sura ya Nne

Sura hii imejadili matokeo ya data zilizokusanywa maktabani na uwandani kwa kuzingatia malengo mahsusi matatu na maswali matatu yaliyoongoza utafiti huu. Matokeo ya mjadala wa utafiti yaliyojadiliwa katika sura hii kulingana na malengo hayo ni mbinu walizotumia watafsiri Edward FitzGerald na Shaaban Robert katika kufanya tafsiri zao. Utafiti umegundua mbinu hizo ni uzingatizi wa umbo la matini chanzi, maudhui, utamaduni wa jamii lengwa na mazingira ambapo tumeona watafsiri hawa walitumia mbinu hizi katika kufanya tafsiri zao. Jambo jingine lililoangaliwa ni kufanana na kutofautiana kwa tafsiri mbili za *Utenzi wa Omar Khayyam*. Mambo yaliyojitokeza katika utafiti ni kufanana katika mbinu za kufanya tafsiri, maudhui na kufanana katika mtindo na katika nia za watafsiri kuzitafsiria jamii zao. Pamoja na kufanana utafiti uligundua kunakutofautiana kwa tafsiri hizi ambapo kuna tofauti za kiutamaduni, kimazingira, na tofauti za kiisimu. Pia, sura hii ilianguka sababu za kuwapo kwa mwachano wa tafsiri mbili za *Utenzi wa Omar Khayyam*. Sababu zilizojitokeza kusababisha mwachano huu ni ugumu wa kutafsiri utanzu husika, tofauti za kiisimu, kiutamaduni na tofauti ya nyakati

SURA YA TANO

MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

5.1 Utangulizi

Sura hii imejadili muhtasari wa tasnifu. Pia, imeongelea hitimisho la utafiti huu na utoshelevu wa nadharia. Aidha, katika sura hii yamezungumzwa maoni ya mtafiti juu ya utafiti uliofanyika na mapendekezo kwa tafiti zijazo.

5.2 Muhtasari wa Tasnifu

Tasnifu hii ilichunguza tafsiri katika ushairi kwa kulinganisha na kulinganua tafsiri mbili za *Utenzi wa Omar Khayyam*, ile ya Kiingereza ya Edward FitzGerald na ile ya Kiswahili ya Shaaban Robert. Tasnifu hii iliongozwa na malengo mahsusi matatu amabayo ni kuchunguza mbinu zilizotumiwa na watafsiri Edward FitzGerald na Shaaban Robert katika kutafsiri *Utenzi wa Omar Khayyam*, kulinganisha na kulinganua tafsiri mbili za *Utenzi wa Omar Khayyam* ile ya Kiingereza ya Edward FitzGerald na ile ya Kiswahili ya Shaaban Robert na kutathmini sababu za kuwapo mwachano kati ya tafsiri hizi mbili za *Utenzi wa Omar Khayyam*.

Sura ya Kwanza imeanza kwa kutoa ufafanuzi wa istilahi muhimu zilizotumika katika utafiti huu. Istilahi zilizofafanuliwa ni tafsiri, mfasiri, ulinganisho na ulinganuzi, matini chanzi, matini lengwa, tafsiri nzuri/mbaya na matini za kishairi. Aidha istilahi zingine kama lugha chanzi, lugha lengwa, utamaduni, itikadi, mila na desturi, mazingira, mtindo, muundo na jamii ya watafsiriwa zimefafanuliwa. Pia, umeelezwa usuli wa tatizo la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti na manufaa ya utafiti.

Sura ya Pili imezungumzia mapitio ya maandiko na kiunzi cha nadharia ya utafiti. Maandiko hayo yamegawanywa katika makundi yanayojumuisha maandiko kuhusu

umuhimu wa tafsiri na maendeleo ya tafsiri ulimwenguni, maandiko kuhusu tafsiri katika fasihi na maandiko kuhusu tafsiri katika ushairi na changamoto zake. Pia, kuna maandiko kuhusu *Utenzi wa Omar Khayyam* na tafsiri zake na maandiko kuhusu kulinganisha na kulinganua matini za kifasihi. Maandiko hayo ndiyo yaliyosaidia kubainisha mapengo ya utafiti huu. Aidha, sura hii ina kipengele cha kiunzi cha nadharia ya utafiti, ambapo mtafiti alitumia nadharia za ulinganisho kama nguzo ya kusimamia katika utafiti wake.

Sura ya Tatu imeeleza methodolojia ya utafiti iliyotumika. Sura hii ina vipengele kama vile usanifu wa utafiti, eneo la utafiti, walengwa wa utafiti na jamii ya watafitiwa. Aidha, vipengele kama vile usampulishaji na sampuli iliyotumika, ukusanyaji wa data, njia na zana za kukusanyia data na mchakato wa ukusanyaji wa data vimefafanuliwa. Sura hii pia, imeelezea uchanganuzi wa data, itikeli ya utafiti, uhalali na uthabiti wa matokeo ya utafiti na mipaka ya utafiti. Nadharia za ulingafu ndiyo zilizotumika katika ukusanyaji, uchambuzi na uchambuzi wa data za utafiti. Hivyo basi, nadharia ya ulinganifu wa kidhima na ile ya ulinganifu wa umbo la matini zilitumika. Misingi mikuu iliyozingatiwa ni tafsiri kwa maana ya matini lengwa kufikia usambamba wa kimaudhui na matini chanzi na kulingana kwa umbo la matini chanzi na matini lengwa. Pia, sura hii imezungumzia changamoto zilizojitokeza katika utafiti na namna zilivyotatuliwa.

Sura ya Nne imeanza kwa kueleza muhtasari wa tafsiri ya Kiingereza na tafsiri ya Kiswahili ya *Utenzi wa Omar Khayyam*. Pia, sura hii imejadili mbinu zilizotumiwa na Edward FitzGerald na Shaaban Robert katika kufanya tafsiri. Utafiti umegundua mbinu hizi ni uzingatizi wa umbo la matini chanzi, maudhui, utamaduni wa jamii ya lugha lengwa na uzingatizi wa mazingira. Aidha kumejadiliwa kufanana na kutofautiana kwa tafsiri mbili za *Utenzi wa Omar Khayyam*, ambapo mambo

yanayofanana na kutofautiana katika tafsiri hizi yamebainishwa. Mambo yanayofanana katika tafsiri hizi nikufanana katika mbinu za kufanyia tafsiri, maudhui, mtindo na kufanana katika nia ya watafsiri ya kutafsiria jamii zao. Mambo yanayotofautisha tafsiri hizi ni tofauti za kiutamaduni, kimazingira na tofauti za kiisimu. Mwisho, kumejadiliwa sababu za kuwapo kwa mwachano wa tafsiri za *Utenzi wa Omar Khayyam*. Sababu zilizo jadiliwa ni ugonu wa kutafsiri utanzu husika, tofauti za kiisimu, kiutamaduni na mihula tofauti ya nyakati.

Sura ya Tano imeanza kwa kueleza muhtasari wa tasnifu, utoshelevu wa nadharia iliyotumika katika uchambuzi wa data na matokeo ya utafiti. Pia, imeeleza mchango mpya uliobanika katika utafiti huu pamoja na mapendekezo kwa tafsiri zijazo.

5.3 Hitimisho

Sehemu hii inaeleza utoshelevu wa nadharia, mchango mpya uliopatikana kutokana na utafiti huu, maoni ya mtafiti juu ya utafiti uliofanyika na mapendekezo kwa tafiti zijazo.

5.3.1 Utoshelevu wa Nadharia Iliyotumika

Katika kukamilisha utafiti huu, nadharia zilizotumika ni ulinganifu wa kidhima na ile nadharia ya ulinganifu wa kiumbo au aina ya matini. Misingi ya nadharia hizi imetumika katika kukusanya data, kuchambua, kuchanganua na kutoa matokeo. Uchambuzi wa data ulizingatia misingi miwili mikuu ya nadharia hizi. Msingi wa kwanza ni tafsiri kufikia usambamba wa kimaudhui kati ya matini chanzi na matini lengwa. Usambamba huu uliangaliwa katika mbinu walizotumia watafsiri hawa kutafsiri *Utenzi wa Omar Khayyam*, kufanana na kutofautiana kwa tafsiri na tathmini ya sababu za mwachano wa tafsiri hizi. Msingi wa pili ni tafsiri kuzingatia

aina au umbo la matini chanzi. Katika msingi huu kuliangaliwa kama watafsiri hawa walizingatia umbo au aina ya matini chanzi wakati wa kutafsiri.

5.3.2 Mchango Mpya wa Tasnifu

Utafiti umeibua michango mipya ifuatayo: Mosi, kupata njia mpya na mitazamo bora kabisa ya kuzitafiti na kuzishughulikia kazi za mshairi Omar Khayyam. Mshairi huyu anazo kazi nyingi sana katika uga huu wa ushairi zilizotafsiriwa kwa lugha mbalimbali ambazo hazijatafsiriwa katika Kiswahili. Pili, kutumia nadharia za ulinganifu wa kidhima na ulinganifu wa aina za matini kuna rahisisha kuzifahamu vizuri tafsiri, hasa tafsiri ya tafsiri. Kwa hiyo, ni vema kwa watafiti kutumia misingi ya nadharia za ulinganifu ili kuifahamu vema tafsiri. Tatu, wanajamii, wasomaji, na watafiti wamepata kumwelewa mtunzi maarufu wa mashairi Mwajemi Omar Khayyam. Nne, kufahamu mbinu mbalimbali zilizotumika katika kutafsiri utenzi huu ambazo zinaweza kutumika kutafsiri matini za kifasihi hasa ushairi. Pia, zimeoneshwa changamoto za kutafsiri ushairi na namna ya kukabiliana nazo.

5.3.3 Mapendekezo kwa Tafiti Zijazo

Tasnifu hii imekuwa chachu kwa wengine kufanya utafiti katika kazi za Omar Khayyam hasa katika kona ya tafsiri. Utafiti huu ulijihusisha na kulinganisha na kulinganua tafsiri mbili za *Utenzi wa Omar Khayyam* hivyo, haukugusia vipengele vingine. Hivyo basi, utafiti huu umeacha mapengo kadhaa yanayohitaji kutafitiwa na watafiti wengine wajao. Mtafiti anapendekeza tafiti zingine zifanyike katika maeneo yafuatayo:

- a) Kuchunguza mhamo wa kimaudhui (uchujufu) wa kimaudhui katika tafsiri ya tafsiri. Hii ni kutokana na kazi mbalimbali kutafsiriwa kwa zaidi ya lugha

moja kwani tumeona kadri matini inavyotafsiriwa baadhi ya mambo huachwa au hujuchushwa.

- b) Kuchunguza tofauti za kimsingi juu ya mbinu za kutafsiri ushairi na kutafsiri tanzu zingine za fasihi. Hii ni kwa sababu katika utafiti huu tumegusia kidogo ugumu uliopo katika kutafsiri ushairi ukilinganisha na kutafsiri tanzu zingine.
- c) Kukusanya na kuchambua kazi mbalimbali za mshairi Omar Khayyam. Hii ni kwa sababu tumeona kuwa Omar Khayyam ana kazi nyingi za ushairi lakini hazijulikani vema kwa jamii ya Waswahili.
- d) Kuhakiki tafsiri ya Kiswahili ili kuona inavyofanana au kuachana na kazi asilia ya Kiajemi.

MAREJELEO

- Basnett, S. (1993). *Comparative Literature. A critical Introduction*. Oxford: Blackwell.
- Biblia. (1997). *Maandiko Matakatifu Pamoja na Itifaki*. Dodoma: The Bible.
- Catford, J. C. (1965). *A Linguistic: Theory of Translation*. Oxford: Oxford University Press.
- Chuachua, R. (2011). *Itikadi katika Riwaya za Shaaban Robert*. Dar-es Salaam: TATAKI.
- Chuachua, R. (2016). *Falsafa ya Riwaya za Shaaban Robert na Euphrase Kezilahabi katika Mukadha wa Epistemolojia ya Kibantu*. Tasnifu ya Shahada ya Uzamivu Katika Fasihi ya Kiswahili. Chuo Kikuu cha Dodoma. (Haijachapishwa).
- Dominique, J. (2012). *Foundational Texts of World Literature*. New York: Peter Lang.
- Encyclopedia Britanica. (2017). *Edward FitzGerald British Author*. Retrieved at 17/8/2017 from www.britanica.com/biography/edward.
- Faiq, S. (2004). *Challenges of Translation from Arabic*. In: Faiq (Ed). *Cultural Encounters in Translation Arabic* (pp 1 -13) Clevedon Multilingual Matters.
- Feruz, S. M. (2011). *Challenges of Translation at The Interface of Culture*. The Case of the Play; Nitaolewa Nikipenda. Unpublished Dissertation of Masters of Arts in Linguistics. University of Dodoma.
- FitzGerald, E. (1859). *The Rubaiyat of Omar Khayyam*. Adelaide: The University of Adelaide.
- Gromova, N. (2004). Tafsiri za Fasihi. Mpya za Kirusi katika Kiswahili. *Swahili Forum II*.
- Jilala, H. na Wenzake (2016). *Nadharia za Tafsiri, Ukalimani na Uundaji wa Istitlahi*. Dar es Salaam: Daud Publishing Company Ltd.
- Kabugi, C. M. (1982). *Nitaolewa Nikipenda*. Nairobi: Sunlitho Ltd.
- Kamegere, F. (1967). *Shamba la Wanyama*. Nairobi: East African Publishing House.
- Kelly, L. G. (1979). *The True Interpreter. A History of Translation Theory and Practice in The West*. Bristol: Basil Blackwell.
- Kipacha, A. (2003). *Lahaja za Kiswahili*. Dar es Salaam: Chuo Kikuu Huria cha Tanzania

- Kumar, K. (2013). *The Making of English National Identity*. London: Cambridge University Press
- Larson, L. M. (1984). *Meaning based Translation*. London: University Press of America.
- Lois, B. (2014). *Nomadis in Postrevolutionary Iran: The Qashqai in an Era of Change Routledge an Ethnic Persian adheres to Cultural Systems Connected with other ethnic Persians*. Tehran: Islamic University Press
- Makacha, R. D. K. na Wenzake (2013). *Kitangulizi cha Fasihi. Nadharia na Mbinu*. Dar es Salaam: TUKI
- Makaryk, I. R. (1993). *Encyclopedia of Contemporary Literary Theory: Approaches, Scholars, Terms*: Canada: Toronto University Press.
- Malagwa, P. S. (2012). "Mbinu mbalimbali za Kutathimini Tafsiri". Katika *Kioo cha Lugha Juzuu*. 10. Dar es Salaam: Taasisi ya Taaluma za Kiswahili.
- Masamba, D. P. B. (2000) "The Handling of Foreign Names and abbreviations (Acronyms)" in *Kiswahili Translation*. Journal of Asian and African Studies, 59233, 238.
- McCarthy, J. H. (1889). *Omar Khayyam. Rubaiyat of Omar Khayyam*. London: Trinity College Publication.
- Mkinga, S. (2005). *Changamoto katika Kufasiri Dhana za Kiutamaduni. Mifano Kutoka Kitabu cha Mwana Mdogo wa Mfalme*. Tasnifu ya Shahada ya Uzamili Katika Kiswahili. Chuo Kikuu cha Dar es salaam. (Haijachapishwa).
- Mligo, E. S. (2012). *Jifunze Utafiti: Mwongozo Kuhusu Utafiti na Uandishi wa Ripoti Yenye Mantiki*. Dar es Salaam: Ecumenical Gathering (EGYS).
- Mshindo, B. H. (2010). *Kufasili na Tafsiri. Nadharia na Mbinu*. Zanzibar: Chuo Kikuu cha Chukwani.
- Msokile, M. (1996). *Misingi ya Hadithi Fupi*: Dar-es-Salaam: Dar es salaam University Press.
- Msokille, M. (1991). *Uchambuzi na Uhakiki – Karibu Ndani*: Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.
- Mulokozi, M. & Kahigi, K. (1982). *Kunga za Ushairi na Diwani Yetu*. Dar-es Salaam: Tanzania Publishing House.
- Mundy, J. (2001). *Introducing Translation Studies. Theory and Applications*. London: Routledge.
- Mungai, M. N. (2005). *Ubunifu wa Mtafsiri. Tamthiliya ya Masaibu ya Ndugu Jero*: Tasnifu ya MA. Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa).

- Mwansoko, H. J. M. (1996). *Kitangulizi cha Tafsiri. Nadharia na Mbinu*, Dar-es-Salaam: TUKI.
- Mwansoko, H. J. M. (2013). *Kitangulizi cha Fasihi. Nadharia na Mbinu*. Dar es Salaam: TUKI.
- Nafisi, S. (2006). *Hakim Omar Khayyam. Tehran: Namak Publishing Company Ltd.*
